Maswali na Majibu Juu ya Waebrania, Sehemu ya III

. . .kuwa hapa Maskanini tena usiku wa leo, kutumainia katika huu ushirika wa ajabu na kuabudu katika Neno la Mungu ambalo limetolewa kwetu bure. Nasi tuna. . .twapenda kuwa washirika wa baraka hizi.

554 Nami natumaini tu kuwa Mungu atatubariki usiku huu kama alivyofanya asubuhi hii, kwa ujumbe wa asubuhi. Nami nilikuwa tu naongea na jirani yangu, Bi-Wood, muda mchache uliopita, nasi tulikuwa tukizungumza pamoja, na Bw. Wood na wengineo. Nami naamini kuwa hayo ndiyo mahubiri bora zaidi ya Ndugu Neville kati ya yote mazuri amehubiri, hayo ndiyo yalikuwa bora zaidi kwangu kuliko yo yote amewahi kuhubiri. Bila shaka nalipenda na kufurahia hayo mahubiri ya ajabu. Na yalinipa moyo na yakanipogoa. Kwa hivyo nina—napenda kukubali ukweli, mwajua. Kwa hivyo, kuhusu ujasiri, mwajua, kuwa na ujasiri, na jinsi ya ku-. . .Daudi alikuwa pale, na jinsi yeye. . .Alipokuwa katika hilo jaribio kuu, badala ya kusema, "Vema, nitakwenda kufanya hili, Bwana, unisaidie tu," yeye alingoja, akaenda akumwuliza Bwana atende nini. Yeye alileta naivera, mwajua, na kusema, "Sasa tusimame na kumwuliza Mungu, "Yatupasa kufanya nini katika mzozo huu?" Ee, hilo lilikuwa nzuri sana. Hilo lilikuwa na vitamini sana kuliko majumba yote ya madawa tuliyo nayo nchini. Naam, bwana, hilo bila shaka linakuimarisha sana.

555 Sasa, usiku huu, hatu—hatukusudii kukawia kupita usiku wa manane, tukiweza, juu ya maswali haya. Kwa hivyo tuta—tutayaingilia, moja kwa moja. Ni kumalizia kwa maswali hayo, na kila wakati nianzapo kuyamaliza. . .(sasa, Dada, Hattie, sikukusudia hilo, wajua hilo. Ni—nilisema tu hilo, ona, na, vema). Lakini nilipata magumu sana hapa toka kwa mhudumu fulani, na ni magumu sana kujibu. Mwajua, hao wahubiri, huyachunguza-chunguza katika Biblia na kujaribu kupata majibu yao wenyewe kabla hawajakuuliza, mwaona. Na ndipo. . .na haya yananasiwa kwenye ukanda, yamwendee rafiki yangu mhuduma, kule Georgia aliye na maswali muhimu sana manane ya Biblia hapa ambayo ni magumu, magumu mno.

556 Na sasa, hili juma lijalo, msisahau na mtuombee.

557 Na mke wangu amepata nafuu; ameamka sasa, na alisaidia kupika, leo. Marafiki zetu wapendwa toka Canada, Ndugu, Dada Sothmann, wako hapa wametutembelea, nasi hakika twathamini kutembelewa nao. Na mke wangu akijua wanakuja,

naam, yeye angeamka apate kuwakaribisha na kushirikiana na hawa watu wakristo wapendwa. Tuna furaha kuwa na Ndugu Freddie pamoja nasi usiku huu, yeye alikaa na . . . Mkewe alikuwa hapa asubuhi hii, lakini naamini alikaa na . . . la, naam, ako pamoja na Meda ili awe pamoja naye tunapokuja humu, kwa kuwa najua tutakawia kidogo usiku huu, ni ushirika na kutawadha miguu. Kwa hivyo tuna furaha kuwa nao pamoja na wageni.

558 Sasa, kabla hatujaanza kujaribu kujibu maswali . . . Na kumbuka tu kuwa na—naweza kukosea, mwaona. Si—sidai kuwa sahihi kwa kila kitu nifanyacho. Na—najaribu kuwa sahihi, bali labda ni—nimekosea. Na—na kama nimekosea, basi mnisameheni tu, nami naomba Mungu atanisamehe, pia, kwa sababu sikusudii kukosea. Sijaribu kuyajibu tu kwa ku- . . . au jinsi mimi . . . kwa dhuluma, najibu vizuri nijuavyo, ona. Na kama yabidi nigeuze mawazo yangu kuhusu swali la Biblia, nadhani sina budi kufanya hivyo. Yatupasa kuyageuza, wakati wo wote, Neno la Mungu linenapo; kwa kuwa ni Neno la Mungu.

559 Na sasa, nadhani tutaombea tena wagonjwa usiku huu, kama kawaida. Na wakati mwingine unashangaa tu; unachukua tu kundi ndogo kama hili, dogo zaidi, ee, Maskani madogo hapa, na wakati mwingine hupati matokeo ambayo ungetaka kuona. Lakini jambo ni kwamba, kile unachotenda, unapata watu mia mbili. Na moja ya mikutano mikubwa, labda unapata watu elfu tatu hadi elfu kumi, mwaona, na—na labda zaidi. Kwa hivyo, hivyo ndivyo ilivyo, mara kwa mara unapata umati mkubwa mno. Lakini usiku huu, nilikuwa tu nikijibu . . . Kwa kuwa simu yetu hulia baada ya kila dakika chache mchana kutwa na sehemu ya usiku.

560 Je, huyu ni Bi, Reisert anayeketi hapa, ninayemtazama? Biblia yako, dada, Dada Wood anayo nyuma kule. Nilikuletea asubuhi hii, nami—sikukupa. Na si—sikukuona asubuhi hii, na Bi Wood anayo.

561 Kwa hivyo kujibu simu na kusikia ma—mambo makuu yaliyofanyika. Bibi fulani alinipigia simu akasema, "Ndugu Branham, nilikuwa kwenye mkutano *fulani* nami nimekuwa nikiugua ugonjwa *fulani* kwa muda mrefu. Na, wajua, wewe ulinena kule, na ku . . . Kasema, "Nusura nizirai. Ilirudisha uhai wangu." Na kasema, "Na sijaugua tena tangu hapo."

562 Na mwanamke mmoja akaingia na kusema . . . Naamini yeye yuko hapa usiku huu, au angesafiri kwa motokaa toka Bedford, naamini, au mahali fulani kule. Mwana wao alikuwa ndani humu, naamini, aliyekuwa na ugonjwa wa moyo, mgojwa sana. Na alikuwa ameketi hapa mkutanoni, na—na Bwana akaja na kumgusa . . . kamwambia mvulana huyo kuhusu magonjwa yake, na ilikuwa vigumu kwake kuinua mkono wake, na ugonjwa wa moyo, na mkono wake wote umepooza, na moyo wake hivi.

Na mara akaingia moja kwa moja garini na kuendesha hadi nyumbani, hajasumbuliwa nayo tena, je, bibi yule amefika humu toka Bedford? Uko hapa? Ndi—ndiye huyo kule nyuma. Naam, ndiyo kwanza anipigie simu muda mchache uliopita.

563 Ndipo kuna mwanamke aliyenipigia simu toka chini kule Evansville. Naye hangefika hapa kwa kuwa ako mbali sana, hakujua tungekuwa na ibada ya uponyaji usiku huu. Naye akasema, "Ndugu Branham, nilikuwa katika mkutano wa kule Evansville," na kasema, "ulitazama makutano na kusema... kaniambia mimi ni nani, na yale nimetenda, na ugojwa wangu, na mengineyo." Naye alisema, "Nilikuwa nimeugua ugonjwa wa pumu na ilinibidi kuchoma dawa ya pumu na kadhalika chumbani tangu nilipokuwa msichana mdogo." Kasema, "Hiyo yapata miaka miwili iliyopita, sijawa na maradhi yo yote tangu wakati huo." Ona?

564 Na kwa wale walio hapa usiku huu, ambao hawakuwako asubuhi hii kufurahia ule ushuhuda; nilikuwa kule kwenye soko dogo, kununua mtoto wa bandia, jana. Naam, hakuwa wangu, ona. Huyo alikuwa wa msichana wangu mdogo, Rebeka, pale. Na—na Sara angeenda mahali, mahali fulani, leo. Baadhi ya wenziwe shuleni walikuwa na mkutano, au maulidi au cho chote kile, naye akampelekea zawadi dogo; nami nilikuwa namunulia kitoto bandia, kikubwa hivi. Mama fulani akaja pale, kasema, "Wanikumbuka?"

565 Nami nikasema, "Sidhani nakukumbuka."

566 Na ikawa kwamba alikuwa jamaa ya Ndugu Neville hapa, ambaye kwamba... Nilipokuwa njiani kwenda Sweden, wao... Yeye akaingia humu, akiwa na mvulana mdogo katika gari la kusukumwa, kama tu maskini Edith hapa, na maskini mtoto yule alikuwa na kansa, kivimbe cha kufisha ubongoni. Na kichwa chake kimeinama chini, naye...na madaktari walikuwa wamebashiri angeishi majuma matatu tu. Wao walikitoa na kukipima, na kuona kilikuwa...kilikuwa... kilikuwa nini, na kampa tu muda wa majuma matatu kuishi. Nao iliwabidi kumtembezea katika kiti cha kusukumwa, na ndipo wakamweka kwenye machela alipoingizwa mle chumbani na kumfanyia uchunguzi, ndiposa wakamrudisha tena. Nami nikaenda kumwombea maskini mvulana yule, na kumsihi Bwana amponye. Na siku iliyo iliyofuata, walipompeleka tena kule, kasema, "Sitaki hicho kiti cha kusukumiwa."

567 Akaingia garini na kubebwa, naye daktari akakunjua machela, kasema, "Sitaki machela hayo."

568 Akakimbia mle na kuketi, daktari akamchunguza, akasema, "Vema," kasema, "badala ya majuma matatu nitakupa miaka mia moja na minane." Angeishi.

569 Na jana, yule mama alikutana nami. Na huenda yuko hapa, nijuapo, usiku huu. Na mvulana yule alikuwa kule nje akicheza

mpira, kijana sasa. Ile kansa ya kufisha iliyomelea ubongoni, na hiyo yaonyesha tu . . .

570 Ee, maelfu ya mambo, ona. Mungu hawezi kushindwa. Hawezi kushindwa kamwe.

571 Ndugu John, Je, jicho lako ni bora, Ndugu? Yeye alipata ajali, alikuwa akipigilia msumari nao ukangonga jichoni. Nasi sote tulikuwa tunamwombea Ndugu John O'Bannon, ndugu yetu toka Louisville aliyepata ajali ya msumari uliongonga jicho.

572 Sasa, maswali haya yametoka kwenye ki—kilindi cha mioyo wa watu fulani: ambao walisoma Maandiko na kupata mambo haya, nao hawa . . . Labda hawawezi kujiridhisha wenyewe, kwa hivyo wanayaleta hapa kusudi tujaribu kuyajibu. Basi mnaona jinsi yanavyotutia hatarini; kwa kuwa, kila usemayo, wanayashikilia kwa dhati. Kwa hivyo basi huna budi kuhakikisha u sahihi, nami . . . .sahihi uwezavyo kuwa. Kwa hivyo basi, jambo la kutufanya tujue kwa hakika tu sahihi, hebu tu tumwuulize Roho Mtakatifu sasa kutufafanulia haya, tunapoinamisha vichwa vyetu.

573 Sasa, Baba uliye Mbinguni, ee, majaliwa jinsi gani kusema "Baba" kwa aliye Muumba mkuu wa mbingu na nchi. Nasi twakuomba tu kwamba Wewe Mwenyewe uyashughulikie maswali haya sasa. Yaliletwa humu kwa moyo mnyofu mno. Mungu, hebu utoke moyoni mwetu, unyofu mkuu mno wa moyo, kuyajibu vizuri sana tujuavyo; tujalie.

574 Na neema zako zitulie juu ya kila moja wayo. Na kitu fulani kisemwe hapa usiku huu ambacho kitamsaidia kila mmoja aliye hapa. Na tuondokapo, baada ya kuombea wagonjwa na kupokea ushirika na kadhalika, na tuseme kama hao waliotoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Kwa kuwa twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

575 Sasa, kama ninavyosema kila wakati, haya—haya ni maoni yangu yaliyo bora sana kwayo, na ndipo wakati mwingine huzusha ubishi mdogo. La kwanza hapo, naona ni jambo ambalo, nimesema mbeleni, ambalo limerudishwa tena. Sita . . . nataka kulisoma tena, mkitaka.

65. Adamu na Hawa walipokuwa na watoto wao Edeni, kulikuwako na watu wengine duniani wakati huu? Katika Mwanzo sura ya 5 na kifungu cha 16, Kaini aliishi katika nchi ya Nodi na akamjua mke wake.

576 Sasa, hilo ni—ni swali la ajabu. Sasa, tumefunzwa katika Biblia . . . Na wakati mwingi haya . . . wakati mwingine sisi bila kujali . . . Nilikuwa nikiweka kijikaratasi hapa, na kusema, "Uliza. Jibu swali lo lote la Biblia."

577 Na mtu fulani akasema, "Vema mke wa Kaini alikuwa nani?"

578 Ee, ningelifanyia mzaha na kadhalika, ningesema, "Ee, huyo alikuwa binti wa mama mkwe wake," au kitu kama hicho, mwajua, au—au "Yeye alikuwa Bi. Kaini." Bali hilo halijibu swali hilo. Kuna . . .

579 Kaini pale alikuwa na mke, kwa sababu Biblia ilisema hapa alikuwa naye. Na kama Kaini alikuwa na mke, sharti alimpata mahali fulani. Na hili lingepatana moja kwa moja na haya humu.

Je, kulikuwako watu wengine duniani wakati Adamu na Hawa walikuwa na watoto wao katika bustani ya Edeni?

580 Sasa, ukitambua, katika Biblia ni vigumu kuandika juu ya kuzaliwa kwa mwanamke. Kila mara mtoto mwanamume ndiye wanayeandika habari zake katika Biblia, si mwanamke. Ni shida kutaja kuhusu kuzaliwa kwa mtoto wa kike, katika Biblia. Ama, kwa kweli, sijui kama ningelikumbuka hata pamoja sasa mawazoni, ambapo kuzaliwa kwa mtoto mchanga kumeandikwa; kasema, "Wakazaa wana wa kiume na wa kike."

581 Sasa, Biblia inatoa tu maandiko ambapo watoto watatu tu walizaliwa na Adamu na Hawa, na hao ni Kaini, Habili na Sethi. Sasa, kama hao wote watatu wangekuwa wanaume, kama hakungelikuwako wa kike ye yote aliyezaliwa, ndiposa basi mwanamke pekee (Hawa) alipokufa, uzao wa mwanadamu ungekoma kuwepo papo hapo, kwa sababu hawangekuwa na njia ya ku—kuzaa na ye yote . . . uzao wa mwanadamu kuendelezwa kwa sababu hakungekuwa na wanawake wo wote waliobaki. Hawa angekuwa wa pekee. Lakini, mwaona, hawaandiki ku—kuzaliwa kwa watoto wa kike, katika Biblia, hivyo basi iliwabidi kuwa na wasichana na wavulana pia.

582 Sasa, yule mwandishi wa kale, mmojawapo wa waandishi wa kale sana tuliye nayo, Josephus, anadi walikuwa na watoto sabini, Adamu na Hawa; mmojawapo wa waandishi wa kale sana, "watoto sabini, nao. walikuwa wana wa kiume na wa kike."

583 Sasa, kama . . . Ndiposa kama Kaini alikwenda katika nchi ya Nodi . . . sasa, ukichunguza huyu mwandishi alikuwa stadi, stadi sana alipoandika—hapa. Je, mliona yeye alivyoyanukuu?

Katika Edeni, walipokuwa na watoto wao Edeni . . . sasa, si katika Bustani ya Edeni, huyu mwandishi alijua hilo. Ye yote yule aliyeandika kijikaratasi hiki hapa, alisema, **Adamu na Hawa walipokuwa na watoto wao Edeni . . .**

584 Si katika Bustani ya Edeni kwa sababu wameshafukuzwa kwenye Bustani ya Edeni. Lakini wao walikuwa bado wangali Edeni, na Bustani ya Edeni ilikuwa mashariki ya Edeni. Lakini Edeni ilikuwa kama nchi au—au kile . . . au mkoa, na ndipo Nodi ilikuwa mkoa mwingine au nchi jirani.

585 Sasa, mtu pekee ambaye Kaini angempata, ama kumwoa, hapana budi ingekuwa dada yake mwenyewe. Alilazimika kumwoa. Kwa sababu kulikuwa tu na mume mmoja na mke mmoja ambamo wangetokea, ona, na yeye alilazimika kumwoa dada yake. Naam, hiyo ilikuwa halali siku hizo.

586 Na Isaka alimwoa binamu wake wa karibu, Rebeka, aliyechaguliwa na Mungu. Sara alikuwa dada ya Ibrahimu, damu moja; si kwa mama yake, kwa baba yake. Ona, dada damu moja ambaye—ambaye Ibrahimu alimwoa; mama mbalimbali, ila baba mmoja.

587 Kwa hivyo, mwaona, kuoa katika jamaa moja siku hizo, kabla da—damu haijapungukiwa na nguvu katika ukoo wa mwanadamu, ilikuwa halali na sahihi. Sasa sivyo. Ukimwoa dada yako siku hizi na mpate watoto, labda watakuwa . . . vema watakuwa vilema na kadhalika. Ni vivyo hivyo hata kwa binamu wa karibu na wa mbali, si halali, ona, kwa sababu damu inakuwa nyonge na hafifu.

588 Lakini jambo pekee lililompasa Kaini kufanya, ingekuwa, kumwoa dada yake mwenyewe. Na hapo ndipo hao watoto walipokuwa ambao . . . Alimchukua mkewe katika nchi ya Nodi na akamjua, na kutoka hapo wa—wakaja watoto. Ona, ile . . .

589 Na mkichunguza, toka kwa ukoo wa Kaini walitokea watu werevu. Uzao wa Sethi ukawatoa watu wa kidini, nakusudia, m—mzabibu wenye haki. Papo hapo, hao wawili, walizaa ukoo ule ule tuliomo siku hizi.

590 Mkitambua siku hizi (kwa kumalizia tu swali hili); huo ukoo wa Kaini bado ungaliko, na ule uzao wa Sethi bado ungaliko, wao wote waliendelea tu vile vile. Watoto wa Kaini wako hapa Jeffersonville usiku huu, na watoto wa Sethi wako hapa Jeffersonville usiku huu. Na damu ya ukoo inaendelea kudhoofika na kufifia, bali ukoo huo ungali unasonga mbele.

591 Sasa, tazama, watoto wa Kaini kila mara . . . walikuwa . . . na kabla ule uangamizi wa gharika, walikuwa watu werevu; wanasayansi, wenye kisomo; na wa kidini sana, bali walikuwa kundi lililolaaniwa. Ona? Sasa tazama, wao walikuwa tu kama baba yao Kaini. Kaini, alikuwa mtu wa kidini. Yeye alijenga madhabahu malidadi, na kutengeneza kanisa malidadi, na kujaribu kulifanya lionekane bora zaidi kuliko ile misheni dogo ya Sethi kule chini. Je, mlijua hilo? Bila shaka yeye . . . Yeye alipamba madhabahu yale kwa maua, na kuyapamba, na kuyafanya malidadi; na kutengeneza makanisa makubwa, makuu, ya kuvutia, kwa sababu yeye alidhani kuwa angepata kibali kwa Mungu kwa kufanya hivyo.

592 Na Habili akaenda akamchukua mwana-kondoo mdogo, na akaanza kumvuta hadi madhabahuni, akamweka juu ya mwamba na kumchinja.

593 Na sasa, Mungu akiwa mwenye haki, kama yote aliyohitaji ni kuabudiwa, Kaini alimwabudu Mungu kwa unyofu mwingi kama tu vile Habili alivyofanya. Wote wawili walikuwa wanyofu. Wote wawili walikuwa wakijaribu kupata neema kwa Mungu. Hamna kafiri kati yao. Wote wawili walikuwa waamini kwa Yehova, kabisa. Naam, hapo, hilo latupa jambo la kuwazia.

594 Wengine hapa usiku huu sijawahi kuwaona watu, sijawaona ninyi kamwe hapa kabla, lakini lazima mkumbuke hili, na kuliweka mawazoni mwenu. Ona? Haijalishi jinsi ulivyo wa kidini, hilo halifai kitu. Huenda ukaishi kanisani, huenda ukawa mnyofu daima, hata hivyo umepotea! Ona?

595 Na mnasema, "Vema," mwasema, "wachungaji wetu ni werevu mno, kapitia seminari na kupata elimu bora zaidi. Wao ni wanatheologia, wajua theologia yote—yote na mengineyo. Nao ni werevu, wamefunzwa, wale . . . wateule bora sana tuwajuao." Nao huenda wamepotea!

596 Sasa Kaini, kwa ukoo wake; walikuwa, kila mmoja, wa kidini sana; watu mashuhuri sana; nao walikuwa wanasayansi na madaktari, na wajenzi na madaktari, na wajenzi na wafanyi kazi, na watu werevu. Lakini ukoo huo wote ulikataliwa, tangu Kaini na kuendelea.

597 Na upande wa Habili; wao hawakuwa wajenzi wala wana elimu, wala watu werevu; walikuwa, kwa kadiri, watu wanyenyekevu, wafuga kondoo, na wakulima, watu ambao walienenda tu kwa Roho.

598 Sasa, Biblia ilisema, "Hakuna adhabu ya hukumu kwao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa mwili lakini kwa Roho." Mtu wa kiroho ana nafsi ya kiroho ambayo haiwezi kamwe kufa. Na mtu wa kimwili amezungushiwa mazingara ya kiroho (na ataka kuabudu na kadhalika) bali ni wa kimwili; si asiyeamini, bali mwamini wa kimwili; na watu wa aina hiyo ndio waliokataliwa.

599 Sasa, toka hapo, Kaini alienda na kumwoa mke wake katika nchi ya Nodi. Sasa, haisemi Sethi alimwoa nani, au ambao wengine walioa. Na jambo nzuri sana lake ni kujua kuwa—kuwa, Kaini alioa, tumepata jibu lake. Kwa kuwa ilimlazimu kuoa dada yake, au yeye . . . au kungekuwa na . . .

600 Hakukuwapo wanaweke wengine duniani, lakini walipaswa kutoka kwa Hawa. Yeye ndiye mama yao wote walio hai. Yaani, watu wote waliokuwa hai, yeye alikuwa mama yao. Hiyo ndiyo sababu yeye alikuwa . . . Neno *Hawa* maana yake ni "mama yao wote walio hai." Kwa hivyo yeye akaja na kumzaa mtoto huyu. Naye Kaini akamwoa dada yake mwenyewe, hivyo ndivyo tu nionavyo hayo. Kwa hivyo kulikuwako watu walioishi katika siku hizo, hakika. Ona? Vema, na . . .

> **Adamu na Hawa walipokuwa na watoto wao katika Edeni . . .** sasa tazama, hilo ndilo swali: **Walipokuwa na**

pamoja na watoto wao Edeni, kulikuwako watu wengine duniani wakati huo? La! Kisha katika Mwanzo 5:16 mwaona, Kaini aliishi katika nchi ya Nod na akamjua mke wake, Bila shaka. Ona hilo?

601 Mwanzo 1, ambapo Yeye alimwumba mwanadamu katika mfano Wake, aliyekuwa katika mwili wa Kiungu. Na katika Mwanzo 2, Yeye alimwumba mwanadamu kwa mavumbi ya ardhi, ambaye alikuwa ndiye mtu wa kibinadamu tuliye naye hivi sasa. Ndiposa katika ya 3 kulikuwako kuanguka kule, na akafukuzwa kwenye Bustani ya Edeni; ndiposa hao watoto wakazaa watoto. Na Kaini akamchukua mke wake na akaishi pamoja naye katika nchi ya Nodi, nje, kwa kuwa Mungu alimtenganisha na ushirika wa ndugu yake mwenyewe (kwa sababu ya mauti ya—ya Habili). Na huyo ndiye yule yeye alikuwa naye, dada yake mwenyewe, na akamwoa; ndiyo njia pekee niwezayo mimi mwenyewe, nionavyo jinsi—yeye alivyooa.

602 Sasa, imesemwa. . .Nami natumaini ya kwamba rafiki zangu weusi waliomo humu ndani wataniwia radhi kwa maneno haya, kwa sababu bila shaka si kweli kamwe. Wakati wa kwanza kukutana na mtu ye yote maishani, baada ya kuongoka. . .nilikuwa. . .nilikutana na Ndugu George De Ark, na wengineo kule. Nami nikaenda, na Bwana akaniongoza hata mahali padogo. Nao walikuwa wakiongea kuhusu alikotoka mtu mweusi. Nao walikuwa wakijaribu kusema kuwa mtu mweusi. . .Kuwa Kaini alioa mnyama kama nyani, na kupitia hapo ukatokea jamii ya watu weusi. Naam, huo ni uongo! Hakika, hilo ni kosa! Na msithubutu kuamini hilo. Kwa kuwa hakukuwa na weusi wala weupe, wala wo wote wale, ni jamii mmoja pekee wa watu hata kwenye ile gharika. Ndipo baada ya ghalika na ule mnara wa Babeli, walipoanza kutawanyika, hapo ndipo walipata rangi zao na mengineyo. Wao wote walitoka kwenye nasaba ile ile. Naam. Adamu na Hawa walikuwa baba na mama, kidunia, wa kila kiumbe kilicho hai cha mwanadamu kilichopata kuwa duniani kamwe. Naam. Weusi weupe, wenye rangi ya kijivujivu, kahawia, manjano, hata uwe wa rangi gani, hiyo bila shaka ni mahali uishipo, na jinsi unavyo—unavyo. . . Kama tu. . .

603 Nadhani huenda nikataja hili ninaponena hayo. Watu hapa sasa katika huu ubaguzi na sheria na mambo wanayoidhinisha, nadhani ni upuzi. Naam. Sikiza, waacheni watu hao pekee yao, wanajua wanachotaka. Mungu alimuumba mtu mweusi naye anafurahia hilo. Hakika! Kama Mungu aliniumba mtu mweusi ningefurahia hilo; Yeye angaliniumba mtu wa rangi ya kahawia, ningefurahia hilo; angaliniumba mtu mweupe, ninafuraha; anagaliniumba mtu wa rangi ya manjano, ningefurahi. Mungu alituumba katika rangi zetu, naye alituumba jinsi alivyotutaka, nasi sote tu watoto Wake. Hakika! Nao haiwapasi kuzozana na

kuendelea hivyo. Ni kosa kufanya hivyo. Hawapaswi kufanya hivyo. Mungu alitufanya . . . jinsi tupendavyo.

604 Na mtu mweusi, yeye hataki kwenda nje pale na kuharibu uzao wa—wake wala rangi yake, na kuichanganyisha na weupe na mengineyo kama hayo. Simlamu. Sifanyi hivyo. Mtu mweusi ana vitu ambavyo hata mtu mweupe hana. Hakika! Hiyo ni kweli kabisa. Na Mungu hakukusudia hao kuwa hivyo.

605 Vema, tazama, mtu mweusi ni . . . yeye ni—yeye ni . . . yeye ana tabia yake mwenyewe ambayo mtu mweupe hana kamwe. Yeye ni mkujufu, mtu wa "mtumainie Mungu, usijali mengine." Awe na kitu asiwe nacho, ni mchangamfu haidhuru. Ningependa kuwa na mengi ya hayo usiku huu, bila shaka. Vema, yeye anayo, na hiyo ni mali yake; ama hawataki kuichanganyisha na watu wa rangi nyingine na kuipoteza, Naam hasa.

606 Nadhani mwanamke yule pale Shreveport alitoa mojawapo wa matamshi bora—bora—sana niliyowahi kuyasikia maishani mwangu. Yeye alitoa matamshi na wakayaandika gazetini. Alikuja, akasema, "Jinsi mambo haya yanavyoendelea hapa, katika huu ubaguzi, sitaki watoto wangu waende kwenye ile shule ya weupe." Kasema, "Hawatashughulikiwa jinsi wangalishughulikiwa wangalikuwa na mwalimu mweusi." Mwanamke huyo ana hekima. Yeye alijua anayonena, wanapata elimu bora. Naam. Kwa hivyo nadhani watu hukosea kwa kufanya hivyo.

607 Na ndipo wao husema, "Kaini na Habili . . . " na kadhalika. La, bwana! Rangi haikuhusika. Ni roho ndani humo inayohusika. Naam, hasa.

608 Kwa hivyo Kaini akamjua mke wake, na huyo alikuwa dada yake. Nao . . . akampeleka katika nchi ya Nod, na kukatokea yale makabila makubwa ya duniani: watu wa kidini na waabudu.

609 Na waza leo, rafiki, hebu tulia ukawaze kwa muda mchache. Kuwa kuna makumi ya maelfu mara makumi ya maelfu na maelfu ya maelfu, ya watu waendao kanisani bila shaka, watu waaminifu sana na waliojitolea kabisa kwa hilo kanisa wawezavyo, ambao wamepotea tu jinsi Kaini alivyopotea. Ona? Mungu ndiye achaguaye! Mungu ndiye ateuaye! Ona? Mungu ndiye arehemuye! Udongo hauwezi kumwambia mfinyazi, ni mfinyanzi mwenye mamlaka juu ya udongo. Naam.

610 Sasa hapa kuna zuri sana, linalofuata hapa:

Katika 2 Petro 2:4-2:4.

611 Mtu fulani aliye na Biblia, ambaye angetaka kufungua Maandiko haya upesi sana ninapoyasoma, mkitaka. Na anisaidie hapa, tunapoliendea swali hili.

612 Sasa, kuhusu huyu Kaini na—na kadhalika, kama hayo hayaridhishi sasa, na tuambiwe. Tutafurahia ku . . .

613 Sasa, 2 Petro 2:4. Vema, bwana, hili hapa;

66. Katika 2 Petro 2:4 "Kwa maana ikiwa . . . kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni," basi mbona Kristo aliwahubiri roho waliokaa kifunguni, katika 1 Petro 3:19?

614 Sasa, tumepata Petro 2:4, kwanza. Vema:

> *Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa—aliwatupa shimoni, aka—akawatia katika vinfungo vya giza, walindwe hata ije hukumu;*

615 Sasa, basi hebu tuone katika 1 Petro, hiyo ilikuwa 2 Petro 1 Petro 3:19, sikiza haya. Ndiyo hii hapa, papa hapa. Haya yamekuja sasa hivi, ndiyo sababu sikuyaandika.

> *. . . ambayo kwa hiyo . . . aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri;*

616 Ee, naam, ndiyo hii hapa. Hebu, tuanzie nyuma kidogo, kifungo cha 18;

> *Kwa maana Kristo naye . . . aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, atulete kwa "Mungu; mwili wake wakuawa, bali Roho yake ikahuishwa,*
>
> *Ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri;*
>
> *Watu wasiotii zamani . . .*

617 Rafiki yangu mpendwa, kama utasoma tu kifungu kinechofuata, na hapo iliyaeleza. Ona?

> *Watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja siku za Nuhu, safina iipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani watu wanane, waliokoka kwa maji.* (ona?)

618 Sasa, kama utatambua ndani humu, nadhani mhubiri huyu ana lingine juu ya . . . jambo lingine kuhusu yayo hayo, litajibiwa hivi punde.

619 1 Petro 4 . . . or 2:4, kama ukiangalia, "kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika," hilo *malaika* limeandikwaje? "m" ndogo. Ona? Sasa hapa, "roho wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu," malaika yule yule. Alikuwa mwanadamu; wajumbe, wahubiri, "hakuwaachilia malaika." Mlijua kuwa . . . neno *malaika* latoka kwa neno "mjumbe"? Wangapi wanajua kuwa malaika maana yake ni "mjumbe?" Bila shaka, malaika ni mjumbe, na hakuwaachilia malaika." Ona?

620 Na huku katika Waebrania, mwakumbuka tulijufunza hayo majuma machache yaliyopita, "wale malaika?"

621 Na kule katika Waebra . . . katika Ufunuo, "Kwa malaika wa kanisa la Sardi andika mambo haya. Kwa malaika wa kanisa

la Efeso andika mambo haya. Kwa malaika wa kanisa . . ." kumbuka hayo? Nasi tulifuatilia neno lile *malaika* kule nyuma, na katika kamusi, na kuona kuwa hilo maana yake ni "mjumbe." Ingekuwa "mjumbe wa duniani, mjumbe wa kimbinguni," lile neno *malaika*.

622 Kwa hivyo katika hali hii, kama tukichukua kamusi na kulitafutilia utaona kwamba limetoka kwa "wajumbe, wale wajumbe wa kwanza." Ona, "Ikiwa . . . Ikiwa hakuwaachilia . . . Kwa maana kama Mungu hakuwaachilia wale malaika wasiotii," (Ona?) "na wale viumbe wa kimbinguni," (ona?) "baada ya kungoja . . ."

Sasa tazama, yeye alisema:

> *. . . ikiwa . . . hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu;*

623 Kisha tazama katika 1 Petro tena, 3:19, tazama hii inavyosema sasa.

> *Ambapo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri;*

> *Watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu . . .* (ona, walikuwa wajumbe wa siku hizo, wajumbe) *. . . safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo . . . ndani yake wacheche, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji.*

624 Sasa kama ukiangalia wakati watu hawa walipokuwa Mbinguni. Sasa, hapo katika Ufunuo 11 . . . au sura ya 7, naamini . . . au la, la, ni sura ya 12. Yeye atoa mfano wa mwanamke aliyesimama, mwezi kichwani mwake na jua . . . au, jua kichwani mwake na mwezi chini ya mguu wake. Na lile joka kubwa jekundu likaamka likamla yule mtoto mara tu alipozaliwa naye akachukua mkia wake na kukokota theluthi moja ya nyota za Mbinguni na kuziangusha katika nchi. Je, ulitambua hilo? Sasa hilo halimaanshi kuwa Shetani ana mkia m—mrefu ambao yeye anawafungia watu, lakini "hadithi *alizowahadithia*," na kukokota theluthi moja ya zile nyota. Nyota hizo ni uzao wa Ibrahimu.

Ibrahimu alisema, "Ee . . ."

625 Mungu alimwambia Ibrahimu, "Tazama mbinguni ukahesabu hizo nyota ukiweza."

626 Yeye akisema, "Siwezi."

627 Yeye alisema, "Wala nawe hutaweza kuhesabu uzao wako." Nyota hao.

628 Je, ile Nyota Yenye kung'aa ya Asubuhi ni nani? Yesu wa Nazareti, inayong'aa sana iliyopata kuishi mwili wa kibinadamu. Yeye ni ile Nyota Yenye kung'aa ya Asubuhi. Naye

ni Mzao wa Ibrahimu, kwa njia ya Isaka. Nasi tukiwa wafu katika Kristo, tunachukua Uzao wa Ibrahimu nasi tu warithi kulingana na ahadi.

629 Kwa hivyo zile nyota za mbinguni ziliwakilisha roho za wanadamu hapa. Na lile joka kubwa jekundu (Rumi chini ya mateso yake) lilipokumbatia theluthi mbili za . . . au theluthi moja ya nyota na kuzitupa chini, hiyo ilikuwa kule kusulubiwa kwa Bwana Yesu walipomkataa naye alikuwa . . . na kumtupa nje na hawakumtaka; hapo kulikuwako hiyo theluthi ya zile nyota za kimalaika, viumbe vya kimalaika.

630 Ona, mwilini mwako, ndani yako . . . (tuna swali lingine juu ta hilo, moja kwa moja, kulijibu vema zaidi). Kwa hivyo wakati . . . Ndani yako kuna roho, mtu mwingine. Nje yako ni mtu mmoja, ndani yako kuna mtu mwingine. Kwa hivyo ndani yako ni ya kimbinguni, nje yako ni ya kimwili. Ona? Na hiki kiumbe, kama unaongozwa na Roho, na Mungu, unakuwa mjumbe wa Mungu, au malaika. *Mjumbe* wa Mungu, *malaika* wa Mungu, ni neno lile; huwezi kuitenganisha; mjumbe wa Mungu au, malaika wa Mungu.

631 Je, nani aliye na mamlaka makuu zaidi? Malaika toka Mbinguni au malaika aliye mimbarani? Nani anayo? Yule malaika aliye mimbarani! Paulo alisema, "Ikiwa malaika toka Mbinguni anawajia na kukuhubirieni injili nyingine isipokuwa ile tumekwisha wahubiri, na alaaniwe." Kwa hivyo malaika aliyepakwa mafuta na Roho Mtakatifu na pia na Neno ni wa pili kutoka kwa Mungu. Naam. Mbinguni, mamlaka yake . . .

632 "Mamlaka yote Mbinguni na duniani yamewekwa mkononi Mwangu. Enendeni nami nitaenda pamoja nanyi. Lo lote mtakalolifungua duniani, nitalifunga Mbinguni. Mtakalolifungua duniani, nitalifungua Mbinguni.'"

633 Jamani, laiti Kanisa kuu lililo takatifu, lingelitambua tu mamlaka yake kufanya mambo haya. Lakini kuna mashaka mengi sana na uoga na kutetemeka, wakishangaa kama itawezekana, "Ingetendeka?" Mradi tu hilo liko, Kanisa haliwezi kamwe kusimama wima. Na maongeo ya uoga yatakapotoweka na Roho Mtakatifu ameshika hatamu kabisa Kanisani, ndipo uoga wote umekwisha, nalo Kanisa litaimarika. Ona? Naam, wana kila Kitu ambacho Mbinguni inamiliki. Hao ni mabalozi wa kile Kiti cha Enzi. Bila shaka! Balozi wa Kristo ana mamlaka, na kila kitu alicho nacho Kristo ni mali ya yule balozi. Naye alisema, "Enendeni ulimwenguni kote, ninyi ni mashahidi Wangu akisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu." Na shahidi ni nani? Ni balozi; ni kuja na kushuhudia jambo fulani. Mamlaka yote ya Mbinguni yako mikononi mwako! Ee, mbona tunaketi kitako? Na kanisa ni tasa, nasi tumelala. Ni kwa sababu hatutambui mambo haya.

634 Sasa, roho waliokaa kifungoni (wasiotubu), hawakuwa viumbe vya kimalaika vilivyokuwa—vilivyokuja katika mfano wa Malaika, lakini walikuwa roho za hivyo viumbe vya kimalaika walioanguka tangu kuwekwa misingi ya dunia, nyuma kule ambako vita vilifanywa Mbinguni. Na Shetani na—na lile joka kubwa wakafanya vita, ndiposa . . . au Mikaeli na—na li—lile joka kubwa (na Nyota wa Asubuhi) wakafanya vita. Nyota wa Asubuhi akatupwa nje pamoja na watoto wake wote (malaika wote aliokuwa amewadanganya), na malaika hao wakaja duniani ndipo wangefanyika wanadamu. Na walipofanya hivyo, hapo ndipo "wana wa Mungu waliona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri, wakajitwalia wake."

635 Hao ni wana wa Mungu. Kila mtu aliyezaliwa duniani humu ni mwana wa Mungu. Haijalishi kama yeye ni mwenye dhambi au nini, yeye ni mwana wa Mungu. Ameumbwa katika mfano wa Mungu kwa sifa za Mungu, yeye ameumbwa hivyo. Lakini Mungu mwanzoni alijua ni nani angempokea Yeye na ni nani hangempokea. Kwa hivyo Yeye angechagua tangu awali . . . au si kuchagua tangu awali bali kwa kujua tangu awali Yeye angejua ni nani angeokoka na ni nani hangeokoka, kwa kuwa Yeye alijua ni mtu gani angepokea roho gani.

636 Na wale roho wanaotoka kwenye kile Kiti cha Enzi cha Mungu, na wanaosimama mbele ya Kiti cha Enzi cha Mungu, na wanaishi . . . na mabilioni ya wakati usiohesabika kabla ulimwengu hata hujaanza, katika Uwepo wa Mungu. Je, wadhani hawajui lo lote kuhusu kuabudu? Nao wakashuka na kuingia katika wanadamu, nao wanamwabudu Mungu! Bila shaka, wanamwabudu Mungu; na wana ujuzi wa Mungu na wana akili, na ni wajanja na daima wana elimu, daima. Bali Mungu aliwakataa tangu mwanzo!

637 Hivyo basi marafiki, ufuasi wa kanisa au—au maarifa ya theologia fulani au cho chote kile, haifai kitu. Haina budi kuwa kwamba Damu ya Yesu Kristo na kuzaliwa mara ya pili ndiko kunakokuunganisha Naye kama mtu mmoja. Naam.

638 Mungu, tangu mwanzo alipojua kuwa . . . Mwanamume na mwanamke waliumbwa mmoja, si wawili, wakafanywa mmoja. Walitenganishwa, mmoja akawekwa katika mwili huu na mwingine katika mwili wa Kiungu. Yeye alijua hilo. Kwa hivyo ili kuwathibitishia ninyi hilo; Mungu alipomuumba mwanamke, Yeye hakuchukua mavumbi tena na kumwumba jinsi alivyomuumba mwanamume; Yeye alichukua ubavu toka ubavuni mwa Adamu, naye akawa mtu aliyetoka kwa mwanamume (kwa sababu yeye ni sehemu yake). Mwafahamu sasa? Ona? Naam.

639 Kuna malaika. Na Mungu na yule roho aliyeunganika na Mungu ni Roho mmoja. Hiyo ni kweli. Sasa, Roho wa Mungu aishiye Kanisani, ni Roho atokaye Mbinguni, ambaye Mungu

alimjua tangu kuwekwa misingi ya dunia, aliyekataa uongo wa Ibilisi. Na roho huyo ilimbidi kuchukua mfano wa mwili ili . . . akajaribiwe. Ilimbidi kufanyika mwili kama hawa wengine walivyofanya, na wote wakachukua nira moja. Naye Mungu, mwanzoni, alijua wale roho ambao wangetenda hayo, na ambao hawangetenda hayo. Naam. Shetani ni mwerevu sana hata ame . . . danganya wale wateule, kama yamkini,

640 Kwa hivyo hawa roho, hawa malaika waliohubiri, waliokuwa kifungoni; *malaika,* ukichunguza hapa, ni "m" ndogo ambayo maana yake ni "mwanadamu," malaika, wajumbe hapa duniani. Walifanya dhambi, na njia pekee ambayo wangetenda dhambi ilikuwa kutokuamini! Na njia . . . walikuwa na dini zao wenyewe, nao hawakuamini ujumbe wa Nuhu. Hawakuamini ujumbe wa Henoko. Nao walikataa Ujumbe wao, "na wakahukumiwa," Biblia ilisema walihukuniwa.

641 Henoko aliwatolea unabii akisema, "Bwana yu—yuaja pamoja na maelfu maelfu ya watakatifu Wake."

642 Nao walitabiri. Naye Nuhu akajenga safina, anao wakasema, "Yeye ni mtakatifu anayejigaragaza! Yeye ni mkithiri dini! Hakuna kitu kama mvua kuja." Na miaka mia na ishirini ikapita, naye alikuwa na dini iliyokuwa na wokovu kwake, njia ilitengenezwa ya kuepukia, lakini walilidhishwa na hali zao.

643 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, ya kwamba wanadamu wameridhishwa na hali zao. Lakini kuna njia ya kuepukia, na njia hiyo ni kupitia kwa Yesu Kristo. Naam; kabila lile lile, roho wale wale.

644 Nao walikuwa watu wa kidini kweli kweli, kidini sana, bali wakakosa kupata ile nadhiri ya agano.

645 Ndivyo ilivyo siku hizi. Watu huenda kanisani, na kujiunga na makanisa makubwa, na kujaribu kuwa watu mashuhuri sana mjini. Wanapotaka kujiunga na kanisa, wanaliendea lililo kubwa zaidi mjini, lililo bora sana na linalowaziwa mema mjini. Wanaukosa ule wito umbali gani! Umbali gani wanaoukosa!

646 Na njia pekee utakayowahi—kujua Yesu Kristo ni kwa kupitia kwa ufunuo wa kiroho, si kwa theologia na jinsi usomavyo Biblia. Au wewe ni Christian Science Methodisti, Mashahidi wa Yehova, au cho chote kile; haijalishi u nani, hutalijua kwa Neno, ni Roho wa Mungu amfunuaye Yeye kwako. Ni ufunuo wa kiroho!

647 Wakati Adamu (katika Bustani ya Edeni) na Hawa . . . wakati watoto hao walipofukuzwa, hapa yuaja Kaini na theologia nzuri. Yeye akasema, "Mungu apaswa kujua kuwa tunafanya hili kwa unyofu—nyofu wote wa moyo wangu. Nitajenga madhabahu malidadi, nitaweka maua juu yake, nitaweka matunda juu yake, nitayafanya malidadi vilivyo. Hakika naweza kumpendeza Mungu kwa haya na kumwonyesha ya kuwa ni mnyofu moyoni mwangu." Yeye alikuwa sahihi kadiri Neno lisemavyo; Mungu

alitaka kuabudiwa, akaenda kuabudu. Alitengeneza mahali malidadi pa kuabuduia, kanisa kubwa la jimbo, zuri sana, (kama wanavyoliita siku hizi). Naye akalijenga vizuri, akalitengeneza vilivyo na kuweka madhabahu ndani yake; yeye hakuwa kafiri.

648 Bali habili, kwa Neno la Mungu. . .Biblia haikuwa imeandikwa wakati huo, bali Mungu akamfunulia kwamba si matunda yaliyotutoa kwenye Bustani ya Edeni, Adamu na Hawa hawakula matofaa siku hiyo, ilikuwa ni kujuana kimwili bila shaka kulikokuwa kumewatenganisha, na akajua kwamba waliharibiwa (katika damu ya Adamu), na kwa damu ya yule nyoka aliyeanzisha hayo. Habili, kwa ufunuo wa Kiungu, akaenda na kuchukua mwana-kondoo na kumtoa dhabihu, kisha Mungu akasema, "Naam, ndivyo!" Bila shaka.

649 Waliposhuka chini ya Mlima wa kule Kugeuzwa, Yesu alisema "Watu hunena mimi Mwana wa Adamu ni nani?"

650 "Wengine hunena Wewe U 'Musa', na wengine hunena u 'Eliya, na wengine hunena U Yerenia,' na wengine hunena U nabii yule."

651 Yeye alisema, "Lakini nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?"

652 Petro akasema "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu Aliye Hai."

653 Yeye akasema "Heri wewe Simoni Ba-Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili." (Tazama!) "Si kwa waraka kamwe, barua, si kwa shule kwamwe; haukusoma hayo kamwe katika seminari, haukuambiwa na mtu ye yote. Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda." Naam. Hilo ndilo Kanisa la Mungu Aliye Hai. Naam. Juu ya kanisa. . .Juu ya *ufunuo*, Kanisa hili limejengwa. Ni ufunuo wa Kiungu ambao Mungu amefunua ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, nawe umempokea kama mwokozi wako binafsi, umepita toka mautini ukaingia Uzimani.

654 Na Roho Mtakatifu ana—anatenda na kufanya kazi katika washiriki wa Mwili huu. Hilo ndilo Kanisa! Haijalishi kama ni maskini, na katika misheni, nanyi husimama chini ya msonobari mahali fulani, au ko kote kule, iwe ni katika nyumba ya mtu binafsi, katika mkutano wa faragha, haijalishi liko wapi. Umalidadi na vinginevyo havimvutii Mungu. Ni unyofu wa moyo kwa ufunuo kwamba Yesu Kristo amedhihirishwa kama Mwana wa Mungu, Mwokozi wetu binafsi. Amina!

655 Lo, sisi . . .hamtafikia haya tukiendelea hivyo, sivyo?

656 Hao ndio walio. . .kule Yeye alikoenda; wale malaika: wajumbe, hao wahubiri, hao wenye elimu, hao wajumbe ambao

hawakuamini Nuhu alipoenda kuhubiri kwao na kuwaambia, “Naam, ingieni katika safina hii.”

657 Walisema, “Msikizeni huyu mtakatifu anayejigaragaza. Sikizeni huyo mkithiri dini. Naam, hakuna mvua. Nani aliyewahi kusikia kitu kama hicho? Hasha, jamani, je, hatuna makanisa? Je, sisi si wa kidini?” Naam, walikuwa wa kidini!

658 Yesu alisema kungekuwa na kizazi kilichopita wakati huo, kizazi hicho kingejirudia tena kabla tu ya kule kuja Kwake. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Adamu ajapo. Walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa.” Walikuwa na Reno, Nevada wakati huo, mahali fulani. Walikuwa na kila upuzi walio nao siku hizi; kubishana, na kuchezacheza, na kufanya mzaha, wafanya mzaha na wengineo; wana aina ya utauwa, lakini wanakana Kweli halisi: lile agano, ule Ujumbe wa neema. Mungu akiwatengenezea njia hii na kuwapa watu agano La—Lake, jinsi wangeepuka, ilikuwa na wokovu Kwake, wokovu ulikuwa mahali pa kuepukia.

659 “Wokovu utatufaa nini?” Siku hizi watu husema, “Je, sisi hatuna serikali ya kidemokrasia? Tunahitaji nini?”

660 Sijali tunahitaji serikali ya kidemokrasia jinsi gani, tunahitaji Damu ya Yesu Kristo. Vema! Tunahitaji Kristo. Na furahia serikali ya kidemokrasia; hiyo haifai kamwe kwa wokovu wa nafsi. Bila shaka! Serikali hizo zitakwisha, na kila taifa litapita. Na nimesimama pale...ambapo mafarao walisimama na yakubidi uchimbue futi ishirini chini ya ardhi ili upate viti vyao vya enzi walivyokalia. Mafarao wote na falme zao za dunia hii, na anasa zake zote vitashindwa na vitakwisha, bali Yehova atamiliki milele, kwa kuwa Yeye ni Mungu asiyekufa. Tunasimama imara juu ya ule mwamba, Kristo Yesu, kwa kuwa misingi mingine yote ni changarawe inayozama.

661 Sijali kama ni...falme zitainuka na kuanguka, lakini ee, hakuna lo lote...sijali kama ni...cho chote; hakuna yaliyopo, wala ya yatakoyokuwapo, hakuna (njaa, wala adha wala cho chote kile) kiwezacho kututenda sisi na upendo wa Mungu ulio katika Kristo. Mtu anapozaliwa kwa Roho wa Mungu yeye si kiumbe cha wakati tena, bali ni kiumbe cha Milele. Amina. Yeye amepita toka mautini kuingia Uzimani. Amepita...amepita mambo ya wakati, akaingia Mileleni. Hawezi akapotea kamwe! Na Mungu aliapa kuwa Yeye angemfufua katika siku za mwisho.

662 Kwa hivyo wanaweza kuwa na makanisa yenu yote makubwa, na anasa zenu zote, na yote mnayotaka, na kufanya mizaha yenu michafu na kucheza karata, n na karamu na kadhalika mtakavyo; na wahubiri walioelimika wamesimama kule. Labda yeye aweza kufanya kazi bora zaidi kuliko baadhi ya maskini vijana hawa ambao hawajui A B C zao. Bali nawambieni yaliyo kweli, afadhali nihubiriwe na kijana asiyejua A B C

(ambaye anamjua Kristo) kuliko wanatheologia wote mashuhuri walio na elimu yenu yote ambayo ingaliwaziwa, Hakika!

663 Chini hapa Kentucky si muda mrefu uliopita, maskini kijana ambaye angesoma jina lake mwenyewe kwa shida, alisema Bwana alimwita kuhubiri naye alitaka jumba la shule. Basi, hiyo halmashuri haingemruhusia kulitumia. Mhubiri mashuhuri akaja pale mwenye kipini kwenye jino lake *hivyo*, mtaalamu mwenye shahada ya juu katika dini, naam, walimruhusu atumie shule hiyo. Bila shaka. Akawa na mikutano ya ufufuo kwa majuma mawili, asipate hata mtu mmoja. Na baba yake akarudi, akasema, "Naam, aruhusiwe kuitumia, mimi ni mlipa kodi, nina haki ya mwanangu kuitumia. Na mwanagu anapaswa kuitumia pia."

664 Kwa hivyo yeye alirudi kupata jibu, na baada. . .Wao wakasema asema, "Vema, tutamruhusu alitumie kwa usiku usiopungua miwili." Nao wakamruhusia kwa usiku muwili.

665 Na usiku huo maskini kijana huyo akaenda kule na hata hangesoma Biblia, ilibidi mtu fulani amsomee somo lake, lakini alipoingia jukwaani, alipakwa mafuta na Roho Mtakatifu. Naye alipohubiri, yapata watu ishirini wakaja madhabahuni, na huyo aliyejidai mhubiri alilia alipokuwa akienda Kalvari, madhabahuni.

666 Naam, ndugu, si—si yale ujuayo, ni Yule umjuaye. Hilo ndilo wazo, hiyo inayohitajika, inafaa kumjua Kristo. Kumjua Yeye, ni Uzima, kumkataa, ni mauti.

667 Upesi kwa maswali yetu mengine, swali sasa linalotupeleka kule kule Georgia:

67. Mawe yale yanawakilisha nini. . .yanawakilisha nini katika Ufunuo 21:19 na 20?

668 Mkipenda kuchukua wakati kufunguo Biblia zenu, ambapo hatuna wakati mwingi sana sasa, bali nitajaribu kuyajibu upesi. Ufunuo ishirini na . . . Naamini ni 21:19 na 20. Naam.

669 Vema, ndani humo mtaona ya kwamba yeye alikuwa akinena kuhusu mawe yaliyokuwa jengoni. Na mawe hayo yalikuwa misingi. Kama mkiangalia. . .naamini unayo pale, Ndugu Neville. Na kila jiwe lilikuwa msingi. Si jiwe moja msingi, na mengine. . .Lakini kila jiwe lilikuwa msingi. Kila jiwe lilikuwa msingi daima. Na kulikuwa na mawe kumi na mawili. Na mkichunguza hayo mawe kumi na mawili hutoa kila. . .Kwanza tukianza na yaspi, na akika na kadhalika, ikiwakili kila jiwe.

670 Katika Biblia humo utapata kumetajwa mawe fulani. Mengine yayo mageni kidogo, hujapata kuyasikia. Ukichunguza katika kamusi utaona kuwa ni jiwe lile lile, majina mbalimbali tu; yamegeuzwa.

671 Lakini yanaanza na—na yaspi. Yaspi ilikuwa jiwe la—la Benjamini . . . au jiwe la . . . ee, yule mwana wa kwanza, Reubeni. Jiwe la kwanza lilikuwa Reubeni, ambalo lilikuwa ni yaspi. Jiwe la mwisho lilikuwa Benjamini, lile jiwe la juu kabisa.

672 Sasa haya mawe kumi na mawili ambayo yalijenga msingi wake, hayo—hayo mawe kumi na mawili yaling'inia katika kifuko cha kifuani cha Haruni. Nayo—yalionyesha, yeye alikuwa kuhani mkuu wa haya—wa haya makabila. Kila mojawapo wa jiwe lao la ukoo ndani humo, katika hiki—kifuko hiki. Na watu walipoona kifuko hiki walitambua kuwa Haruni alikuwa kuhani mkuu wa kabila hilo lote, walipoona lile jiwe la ukoo katika kifuko hiki.

673 Naam, kama tulivyoona asubuhi ya leo katika ujumbe wa Ndugu Neville. Na wakati mwingi walileta Urimu Thumimu. Mwaiona imetajwa katika Biblia kama njia waliyoujulia ujumbe wao kama ulikuwa Kweli au la. Mawe hayo, walipoanza kunena yale mtu alisema, nabii alipotabiri mawe yote yalirudisha nuru zao pamoja. Ilisababisha mchanganyiko wa nuru uliochukua yakuti samawi, na yaspi na akiki, na mawe hayo mengine yote yakirudisha nuru zao pamoja. Yalisababisha rangi kubwa malidadi za upinde wa mvua ambao uliunganisha kitu hicho chote pamoja.

674 Sasa—sasa siku ile ambayo Urimu Thumimu iliondoshwa pamoja na ukuhani huo, sasa Biblia hii ndiyo Urimu Thumimu ya Mungu siku hizi. Na mhubiri anapohuhiri, haipaswi kuwa mahali padogo tu hapa, na hapa pawe ndipo tu yeye awekapo tumaini lake; lazima Biblia nzima iangazie ujumbe ule mtu huyo mtu anaohubiri. Ndivyo ipasavyo. Si mahali pamoja pekee, na kusema, "Vema, Biblia yasema hili." Ee, hakika, inasema mambo mengi sana. Lakini lazima uunganishe yote pamoja. Na Roho wa Mungu ajapo na kuingia katika lile—lile Neno, huliunganisha lote pamoja na kuangaza kwa Nuru moja kubwa mno, na Nuru hiyo ni Yesu Kristo.

675 Sasa, haya mawe kumi na mawili yalikuwa misingi iliyoanzishwa toka kwa Reubeni, na Gadi, na kuendelea hadi kwa Benjamini, makabila kumi na mawili, mawe kumi na mawili. Na mawe hayo kule Hekaluni, katika Yerusalemu mpya itokayo Mbinguni, kila msingi utawekwa juu ya kila mmoja wa wale wazee wetu.

676 Sasa tazama, mkichunguza mawe yale, sasa mtawaona wale, wazee wetu wakionyeshwa katika mahali pengine, katika swali lingine.

68. Eleza—eleza yule wa nne . . . wale wenye uhai wanne wa Ufunuo 5.

677 Ndugu Neville, kama umeyapata hayo hapa karibu, au mmoja wenu, ya Ufunuo 5, tutasoma hili kwa dakika moja hivi

tu. Ni—ni mfano malidadi hapa wa wale . . . hapa, nimepapata mwenyewe, Ufunuo sura ya 5:

> *Kisha nikaona katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi . . . juu ya kile kiti cha enzi kitabu kilichoandikwa ndani na—na—na nyuma, kimetiwa muhuri saba.*
>
> *Nika . . .*

678 Sasa, hapo sipo. Nataka kuendelea tu mbele kidogo, wale wenye uhai wanne. Hebu tuone, kifungu cha 14. Vema, bwana. Sasa twasoma, basi. Sasa hebu tuanzie juu hapa ki—kifungu cha 12, la, nadhani ni— . . . "Na wale wenye uhai wakasema, 'Amina." La, kuna mahali padogo nyuma yake, Ndugu Neville. "Tazama, nikasikia sauti . . . "

679 Hebu tuone, kwa dakika moja hivi, nilikuwa nikipasoma muda mchache uliopita. Ee, ni hapa, hebu tuanzie kifungu cha 6. Kifungu cha 5:

> *Na mojawapo wa wale wazee akaniambia, Usilie, tazama, Simba aliye wa Kabila la Yuda, Shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na zile . . . mihuri zake saba.*
>
> *Nikaona . . . katikati ya kile kiti cha enzi . . . na wale wenye uhai wanne, na katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba, ambazo ni Roho saba zilizotumwa toka . . . katika dunia.*

680 Nawatakeni ninyi mshikilie swali hilo na nisipolipata chini hapa katika dakika moja hivi, nataka ninyi mlirudishe tena, nataka kushughulikia hilo, "zile roho saba zenye yale macho saba yaliyokuwa juu ya yule Mwana-Kondoo." Ee, hilo ni jambo nzuri sana. Vema, twataka kupata swali la ndugu huyu sasa.) Vema, msisahau hilo sasa.

> *Akaja, akakitwaa kile kitabu kitabu katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi.*
>
> *Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za mwana-kondoo . . . kila mmoja wao ana kinubi, . . .*

681 Sasa, hao ndio wale—wale wanne—wale wenye uhai wanne hapa kama ukiangalia. Sasa hebu tuendelea mbele na kusoma mbele kigogo.

> . . . *kinubi* cha dhahabu . . . *vilivyojaa* vitasa na *manukato . . . ambayo ni maombi ya watakatifu.*
>
> *Nao waimba wimbo mpya . . . Wastahili wewe . . .* (na kuendelea na kufanya . . . kuabudu kwa kwote kwa Bwana)

682 Sasa, hawa wenye uhai wanne wa Ufunuo, ukiwachunguza, kila mahali . . . (Ninyi wasoma Biblia, na ye yote atakayesikiza hii tepe iliyonaswa). Hao wenye uhai wanne, walikuwa na nyuso nne; mmoja alikuwa mfano wa mwanadamu, mwingine alikuwa mfano wa ndama, na mwingine mfano wa tai, na mwingine alikuwa mfano wa simba. Nao hawarudi nyuma kamwe, hawangerudi nyuma.

683 Wangapi wanaokumbuka tulipofundisha kitabu cha kale cha Ufunuo miaka mingi iliyopita, nilipochukua karibu miaka miwili hapa kwenye kile Kitabu cha Ufunuo? Watu wengi wa kale wajua.

684 Tazama, hawangerundi nyuma, kwa maana kila upande walikoenda walikuwa wakienda mbele. Walipoenda upande *huu* wangeenda kama simba; wangalienda *huku*, wangalienda kama tai; wangienda *huku*, wangalienda kama ndama. Ona, hawangeenda nyuma, walikuwa wakienda mbele daima.

685 Naam, hao wenye uhai wanne. Sasa kupata hili upesi kwa kuwa sitaki kukawia sana kwa hili. Lakini wale wenye uhai wanne . . . *Mwenye uhai* katika Biblia, huwakilisha "nguvu." Na ukiangalia hawa wenye uhai hawakuwa kule ziwani wala katika bahari mahali fulani wakijitokeza, bali walikuwa penye kile Kiti cha Enzi cha Mungu, nao walikuwa wakimwabudu Mungu. Hao wenye uhai wanne maana yake ni nguvu zilizoinuka kutoka duniani, na hizo nguvu nne zilikuwa zile Injili nne; Mathayo, Luka, Marko na Yohana; hazitofautiani.

686 Na mmoja wao, yule . . . Injili iendapo kama simba, ni kali, ni jasiri; Injili ni jasiri kama simba, na falme kama simba. Ikiuendea uso wa mwanadamu, ni jasiri na erevu kama mwanadamu. Ikienda kama tai, ina mabawa mepesi na umbali wa juu. Ni . . . Mwafahamu ninayokusudia? Ikienda kama ndama, ni farasi mtenda kazi awezaye kuvuta, ni kazi ya ndama kuvuta m—m—mzigo wa Injili. Wale wenye uhai wanne walikuwa zile nguvu nne, ambazo ni: Mathayo, Marko, Luka, na Yohana; zile Injili nne zinazotuingiza katika Uwepo wa Mungu. Hao walikuwa . . .

687 Kama mkiangalia, walikuwa na macho mbele na nyuma, Hao—hao . . . Kila mahali ilikoenda, iliangaza. Waliona kila mahali walikoenda. Na hiyo ndiyo nguvu ya Injili inapoenezwa, yaweza . . . Ina ujasiri wa mwanadamu; ina wepesi wa tai; ina ile—ile—ile—ile nguvu, nguvu ya kuvutia, bebaji mizigo kama ndama; ina u—u—ukali na ujasiri wa simba. Ona, ni zile Injili nne, ambazo ni nguvu nne za Ufunuo, sura ya 4.

Vema, sasa linalofuata:

69. Hawa wazee ishirini na wanne ni akina nani? Vema. (Naamini hiyo ingekuwa kwa ile—ile . . . **Hawa wazee ishirini na wanne ni akina nani?**

688 Sasa hilo ni rahisi, tu, tungelipata. Wale wazee ishirini na wanne walikuwa wameketi mbele ya kile Kiti cha Enzi. Hapo ni katika . . . naamini ni katika kifungu cha 4, ndipo inapopatikana. "Na wakatoka nje . . . Yanipasa ku . . . Hebu tuone, nina . . . 4:10

689 Vema, Ufunuo, sura ya 4, na kifungu cha 10. Naam, tutaifungua.

> *Ndipo hao wazee ishirini na wanne huanguka mbele zake yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi nao humsujudia yeye aliye hai hata milele na milele, nao huzitupa taji zao mbele ya kile kiti cha enzi, wakisema,*
>
> *Umestahili wewe,* Ee *Bwana, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa.*

690 Sasa wale wazee ishirini na wanne. Mzee ni mwangalizi. Sasa, tazama, hao walikuwa wale wazee wa makabila kumi na wawili na wale mitume kumi na wawili. Nao walikuwa wameketi, kumi na wawili upande huu na kumi na wawili upande ule. Kulikuwa na wazee ishirini na wanne, ambao walikuwa: wale wazee wetu upande mmoja, Agano la Kale, wale mitume kumi na wawili upande mmoja, wa Agano Jipya. Je Yesu hakusema, "Mtaketi katika viti kumi na viwili vya utukufu, mikiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli?"

691 Na jinsi misingi ilivyokuwa. Hata kuna mti ndani mle, na mti ulio kila upande huzaa aina kumi na mbili za matunda. Nayo huzaa matunda yake mara moja kwa mwezi, ambayo ni miezi kumi na miwili katika mwaka. Yalizaa aina kumi na mbili za matunda kila mwaka upitao. Kumi na mbili katika hesabu ya "kuabudia," mwona. Na kunao ishirini na wanne, ingekuwa ishirini na wanne, mitume kumi na wawili na wazee wetu kumi na wawili. Wameketi penye kile kiti cha enzi.

692 Vema, sasa kifunguu cha 4 . . . au swali la nne:

70. Ule uzi mwekundu katika Mwanzo 38 uliwakilisha nini?

693 Ule uzi mwekundu, ukichunguza, ulikuwa Yuda. Naye alikuwa na wana wa kiume, na mmoja wa wana wake aliomwoa mwanamke Mkanani. Na huyu mwanamke Mkanani hakupata mtoto ye yote, kisha mwanawe akafa. Ndipo sheria inge . . . mwana aliyefuata ilimpasa kumtwaa mke wa nduguye, akamwinulie uzao yule aliyekufa, Na huyo mtu mwingine hakushirikiana na kufanya kama ilivyombidi. Na Bwana akamuua. Ndipo yeye alikuwa na mwana wa kiume mdogo; kwa hivyo Yuda akasema, "Ngoja hata mwana huyu aendeshe . . . akue, hata umri ambao unaweza kuolewa naye."

694 Naye alipokua hata umri ambao alipaswa kuoa wake za ndugu zake wawili waliotangulia, vema, yeye alipaswa kumtwaa basi, kuwainulia uzao nduguze waliokuwa wame . . . waliokufa.

Yuda hakumpa mwanamke yule (yule mwanamke Mkanani) yule mwana, yule mvulana, na akaacha tu yeye aendelee. Kwa hivyo yeye aliona kuwa alikuwa amekosewa, kwa hivyo akaenda na kujifungia kitambaa usoni mwake, na kuketi hadharani jinsi angaliketi kahaba.

695 Yuda alipitia hapo na kumchukua mwanamke huyo kama mke wake, naye alikuwa kahaba, na akaishi naye. Na akasema, mwanamke huyo akasema, “Vema, utanilipa nini?” Naye . . . mwanamke yule akasema . . .

696 Yeye alisema, “Nitampa mwa—mwana-kondoo.” Akasema, “Vema, nipe rehani kuwa utafanya hivyo.” Kwa hivyo mwanamke huyo alichukua fimbo yake na pete yake ya muhuri na kadhalika, na kuiweka.

697 Na walipomleta yule mwana-kondoo, hawakuweza kumpata kahaba yule, kwa kuwa yeye hakuwa kahaba.

698 Muda si muda, akapata mimba. Na ndipo alipoonekana ni mja mzito, wakamjia Yuda na kumwambia, “Mkweo amefanya ukahaba.” Kasema, “kwa kuwa yeye—yeye ni mja mzito, na vijana wako wote wawili wemekwisha kufa.

699 Yeye akasema, “Vema, ataitwa aje na kuchumwa moto.”

700 Na kwa hivyo mkwewe alituma habari kwa Yuda, naye akasema, “Mwanamume aliyefanya hili, ndiye mwenye fimbo hii na pete hii ya muhuri.” Vema, huyo alikuwa mkwewe.

701 Naye Yuda alisema, “Yeye ni mwenye haki kuliko mimi.”

702 Sasa, yeye alipojua watoto wake wako karibu kuzaliwa, walikuwa mapacha. Na wakati mapacha wale . . . Mtoto wa kwanza kuzaliwa, zile desturi za kale za Kiyahudi, mtoto wa kwanza ana haki ya mzaliwa wa kwanza. Na huyo, kumbuka, alikuwa mtoto wake wa kwanza. Hakuna yeye yote kati ya vijana wale aliyekuwa amepata mtoto ye yote naye. Alikuwa hajapata mtoto hata wakati huu.

703 Na wakati mwanawe wa kwanza alipotokea, ilikuwa mkono pekee. Na mzalisha akaufunga mkono wake kwa uzi mwekundu, kwa kuwa ule uzi mwekundu ulinena kuhusu ukombozi ambao yule mwana wa kwanza wa bikira Mariamu ange . . . angekuwa na ule uzi mwekundu wa ukombozi.

704 Naye alipourudisha mkono wake, yule mwingine akazaliwa kwanza. Naye alipofanya hivyo alisema, “Mbona ulifanya hivyo? Yule mwingine ana haki ya mzaliwa wa kwanza.”

705 Kwa hivyo hiyo ndiyo maana ya Mwanzo 38, mwaona. Ya kwamba yule mwana wa kwanza alisalia hata kule kuja kwa Bwana Yesu Kristo. Ya kwamba yule wa kwanza alikuwa yuangali chini ya sheria ya ukombozi.

706 Mwajua nilisema . . . maskini yule nyumbu, mwajua, nimenena habari zake, kuwa macho yake yalikuwa . . . cho chote

kile, masikio yake yalivunjika, lakini yeye alizaliwa mwenye haki ya mzaliwa wa kwanza. Mwana-kondoo halisi asiye na hatia alikufa mahali pake. Ndivyo ilivyo.

707 Kwa hivyo hiyo ilikuwa kwa ajili ya haki ya mzaliwa wa kwanza. Mwana wa kwanza aliyetoka kwa mama, waliuona mkono ule (na kujua kuwa huenda ukarudi ndani tena). Naye alipoutokeza mkono wake kuonyeshe kuwa yeye alikuwa ameipata, yeye alikuwa wa kwanza, yule mzalisha aliufunga ule uzi mwekundu naye akaurudisha mkono wake. Ona? Lakini, bila shaka, yeye ndiye alikuwa wa kwanza. Hiyo ndiyo ule uzi mwekundu, uzi mwekundu una . . . kokote katika Biblia, maana yake ni ukombozi; ambayo ilikuwa ikielekeza mbele kwa yule mwana wa kwanza anayekuja.

708 Farasi wa kwanza, ng'ombe wa kwanza kuzaliwa, cho chote kile, kila kitu kilichozaliwa kwanza (kijitokezacho) kilikuwa chini ya ukombozi, kilipaswa kikombolewa; kila kitu kilipaswa kukombolewa! Haleluya! Ee, hilo lanichangamsha mimi. Je, mwalifahamu? Cha *kwanza* kilipaswa kukombolewa. Ilikuwa ni sheria. Lihimidiwe Jina la Bwana.

709 Na Yesu Kristo alipozaliwa, Yeye aliukomboa ulimwengu wote. Bila shaka, Yeye aliukomboa. Yeye alikuwa Mkombozi wa kila kiumbe kilichoumbwa duniani. Alikuwa Mkombozi. Na katika . . . ukombozi wote umo ndani Yake, na hakuna njia nyingine iwayo yote uwezayo kupitia kwa kazi nzuri, kwa kujiunga na kanisa, wala cho chote kile; huna budi kuja kwa huo uzi mwekundu, huyo Mkombozi, huyo Mkombozi wa jamaa yetu.

Vema, Sasa lililofuata ni:

71. Ziko wapi zawadi . . . Ni zawadi gani zitakazopelekeanwa kuhusu kifo cha wale mashahidi wawili katika Ufunuo 11?

Ee, Ndugu Palmer, kweli unaweza kuuliza maswali kadha!

710 Sasa, ule ukombozi, hizi nyuzi hapa, hizi nyuzi nyekundu twaona zilimaanisha ukombozi.

711 Sasa swali linalofuata ni:

Ni zawadi gani katika Ufunuo 11?

712 Wakati unakuja . . . sasa hapa tutajibu swali lililojibiwa usiku mwingine, ambalo rafiki yangu mhubiri aliandika kuhusu Wayahudi, jinsi itakavyokuwa.

713 Sasa Wayahudi hawa wana miaka mitatu na nusu waliyoahidiwa. Wangapi wajua hilo? Majuma sabini yaliahidiwa. Kasema, "Masihi atakuja na kukatiliwa mbali katikati." Miaka mitatu na nusu Kristo alihubiri, akauawa katika miaka mitatu na nusu hasa, miaka mitatu na miezi sita Yeye alihubiri.

714 Ndiposa lile chukizo la uharibifu, ule—ule uislamu wa Omar ulinjengwa kwenye Mahali Matakatifu; Mungu alivyosema,

miaka elfu mbili mia tano kabla haijatendeka, ungekuwa umesimama pale. Nabii aliuona, na kuuona, na kusema, “Wange. . .Mataifa wangemiliki pale hadi majira ya Mataifa yatakapotimia.”

715 Sasa bado kungali miaka mitatu na nusu waliyoahidiwa. Ukichunguza, hawa mashahidi wa Ufunuo 11 wanatoa unabii siku elfu moja mia mbili na sitini, miaka mitatu na nusu hasa. Sasa. . .nao walikuwa katika magunia. Sasa, tazama huduma yao, jinsi walivyo. Sasa hawa mashahidi wawili wakauawa.

716 Sasa, ile. . .Hao walirudia Wayahudi baada ya Kunyakuliwa kwa Kanisa la Mataifa. Kanisa la Mataifa laenda Nyumbani kwa ile karamu ya arusi kama Rebeka alivyochukuliwa kwa Ibrahimu pamoja na Isaka na kuolewa. Na Rebeka na Isaka wakapokea mali yote ambayo Ibrahimu alikuwa nayo, yote ilimwendea Isaka. Bila shaka! Na haingekuja kwa Isaka ila kwanza Isaka aoe. Ee, haleluya! Naam.

717 Naye Kristo anakuwa. . .Mungu huishi katika mwili huo mkamilifu, uliotiwa doa, ulioharibiwa kabisa milele na kote mileleni. Yule Mwana-Kondoo na Bibi-arusi watakapofanya arusi Mbinguni, Bibi-arusi ataondoka amemiliki yote. Bila shaka! Isaka na Rebeka walimiliki yote.

718 Na humu sherehe hizi zinapoendelea Mbinguni, za Bibi-arusi, Bibi-arusi wa Kimataifa anapoolewa na yule mtawala (Mwana wa Mungu), Utukufuni; huku wakioana, kunao muda wa miaka mitatu na nusu ambapo. . .Musa na Eliya. . .

719 Ambapo, Musa hakutoweka kamwe. . . .la, mwili wake ulihamishwa. Malaika walimtwaa, walimtwaa, yeye hakuharibika, hakuona uharibifu. Alikuwa mfano kamili wa Kristo. Yeye alikufa nao Malaika wakamhamisha, na hata Shetani hajui ambapo yeye alizikwa, na alijaribu kupingana na yule Malaika Mkuu Mikaeli kuhusu mazishi yake. Hivyo ndivyo ilivyosema Biblia. Mungu alimtwaa katika kunyakuliwa.

720 Na Eliya, alipokuwa akitembea pale, yule nabii wa Mungu alishuka akaenda hadi Yordani, akachukua vazi lake na kuyapiga maji, nayo yakagawanyika kuume na kushoto. Akapanda juu ya mlima. Elisha akasema. . .kasema, “Mbona unanifuata?”

721 Yeye akasema, “Nataka sehemu maradufu ya Roho yako.”

722 Kamwambia, “Umeomba jambo ngumu, lakini ukiniona ninapokwenda.” Akamkazia macho daima.

723 Na baada ya muda mchache, toka Mbinguni kukashuka magari ya moto na Malaika wa moto, farasi wa moto, na Eliya akapanda kwenda juu Utukufuni. Yeye hakuonja mauti, aligeuzwa, hana budi kufa!

724 Na kama utachunguza hawa manabii wawili wa Ufunuo 11, wanafanya jambo lile lile ambalo Musa na Eliya walifanya.

Mwasema, "Ndugu Branham, wakusudia kuniambia kuwa Eliya na Musa bado wangali hai?" Bila shaka!

725 Naam, mbele ya ule Mlima Kugeuzwa . . . .Kwenye Mlima wa Kugeuzwa, kabla Yesu hajaenda Kalvari, ndio hao Musa na Eliya wakisimama pale wakinena Naye. Bila shaka, waliongea naye, hawajakufa bado. Nao hawakufa kamwe; hao ni wanadamu, hawana budi kufa. Kwa hivyo wako tu katika hali ya utukufu wakingojea wakati huo.

726 Ndiposa warudipo na kuhubiri kwa ile miaka mitatu na nusu halisi chini ya upako wa Ubatizo wa Roho Mtakatifu, huku baraka zinapoondolewa kwa Mataifa (na Kanisa limetwaliwa); na lile kanisa baridi la kidesturi linawindwa kama mbwa, na ukamunisti na wafuasi wa Kirumi, nao wanapowindwa na kuuawa. Hao—hao wanauawa wakati huo; hawa manabii wanahubiri kwa miaka mitatu na nusu, na Biblia ilisema kuwa waliuawa katika ile . . . katika njia ya mji uitwao kwa jinsi ya roho, Sodoma na Misri, ambapo Bwana wetu alisulubishwa. Hapo ni kule nyuma Yerusalemu; ona, kule nyuma Yerusalemu, inavyoitwa kwa jinsi ya roho.

727 Nao walikuwa katika njia ya mji kwa siku tatu mchana na usiku. Ndiposa mwishoni mwa zile siku tatu u nusu, roho wa uhai ikawaingia nao wakafufuka. Iliwabidi wafe kama wanadamu wengineo, iliwabidi wafanye hivyo. Na walipowaua wale wahubiri wawili . . .

728 Walihubiri dhidi ya uovu, nao wakauleta moto toka mbinguni. Nani alifanya hilo? Ona? Wakaleta mapigo toka mbinguni, na kupiga nchi upesi kama . . . na kwa wakati wo wote walipotaka kufanya hivyo. Nao wakaleta moto toka mbinguni. Nao walizifunga mbingu ili mvua isinyeshe, kila watakapo. Huyo alikuwa nani? Musa na Eliya hasa. Ndio hao wale mashahidi wawili.

729 Na walipolitesa kanisa, au ulimwengu, kwa mahubiri yao; na kuwapokea tena Wayahudi, na kuwafanya watubu, kuwarudisha wamwamini . . . Wamwonapo Yesu akija kwa ajili ya Bibi-arusi, watasema, "Tazama, huyu ndiye Mungu wetu tuliyemngoja. Huyu ndiye!" Bali Yeye haji kwa ajili yao. Yuaja kwa ajili ya Bibi-arusi Wake. Na Bibi-arusi Wake . . .

730 Yusufu alipokwenda Misri, hakuchukua ndugu zake pamoja naye, lakini alimpata bibi-arusi wake kule. Bila shaka! Bali alipojitambulisha mwenyewe kwa ndugu zake, hapakuwepo mtu. Naam hasa. Naye atakapojitambulisha kwa hawa Wayahudi, hakutakuwako mtu ila Wayahudi. Ndio hao waliomwuua Yusufu, wakisimama pale; na yeye alisema, "Vema, mimi ndimi Yusufu, ndugu yenu." Naye akalia.

731 Nao wakasema, "Sasa tutapata cha mtema kuni, kwa sababu tulimwua."

732 Jambo lile lile. Hao Wayahudi watakuwa na wakati mwingi wa shida kabla ya kule kuja sasa, wa mateso ya kuwarudisha katika nchi ya uenyeji wao. Wakikusanyika kama kundi la kondoo wakirudi kwenye Mlima Karmel kule.

733 Bwana Yesu atakapokuja kwa ajili ya Bibi-arusi Wake, nao watakapomwona, watasema, "Huyo ndiye tuliyemngoja, ndiye huyo!" Atatuzukia, mwenye uponyaji katika mbawa Zake. Naam.

734 Na kanisa, yale masalio ya Wayahudi, watakapowaua hawa manabii wawili, na wawe katika njia za mji ule uitwao—kwa jinsi ya roho Sodomo na Misri, ambapo Bwana wetu alisulubiwa, watapelekeana zawadi wao kwa wao (ulimwengu utafanya hivyo)

735 Sasa, Ndugu Palme, basi. Chunguza historia ya Kirumi na utaona ya kwamba kuna taifa moja pekee ulimwengu ambalo lilipelekeana zawadi kamwe baada ya vita, hilo ni Milki ya Kirumi.

736 Hiyo ndiyo sababu nasema kuwa yule mpinga Kristo atatoka Rumi. Yule mnyama atoka Rumi, hawezi akatoka Moscow. Anatoka Rumi, lile joka jekundu lililosimama karibu na mwanamke yule kumla mtoto wake mara tu azaliwapo. Je, huyo shetani, shetani huyo alikuwa wapi? Alikuwa nani? Kaisari Agosto aliyetoa amri na kuua watoto wote tangu miaka miwili kwenda chini. Lile joka jekundu, lile joka, *mnyama* maana yake ni "mamlaka." Mamlaka ya Kirumi yalimtesa na kujaribu kumpata huyo Mtoto Kristo.

737 Na jambo lile lile! Kila wakati ambapo Warumi, ile Rumi kafiri ya kale ilipopata ushindi mkuu, wangepelekeana mawe mweupe na kadhalika wao kwa wao, zawadi kama hizo, kwa ukumbusho. Kwa hivyo mawe hayo yaliyokuwa. . . jinsi yalivyokuwa, yalikuwa zawadi dogo kati ya kanisa la Kirumi. Bila shaka. Ndivyo hasa. Naam.

738 Nilisimama papo hapo katika Jiji la Vatican na kuithibitisha kwa Biblia. Yule papa amevalia taji yenye sehemu tatu, *Vicarivs Filii Dei,* mambo hayo yote ambayo nimeyasikia na kadhalika, ni kweli kabisa; kundi la kidini linalotawala kila taifa chini ya mbingu, na linafanya hivyo. Ndilo hilo, ndivyo ilivyo.

739 Sina cho chote dhidi ya watu Wakatoliki (la, bwana), hao ni wazuri tu kama ye yote yule, bali dini yao si sahihi kulingana na Biblia hii hii. Kama Biblia hii ni sahihi, wao wamekosea. Wanasema hawaja. . . "Haijalishi Biblia yasema nini, ni yale kanisa lisemayo." Twaamini kuwa Biblia inanena na mamlaka makuu kushinda yote! Bila shaka, ni Neno la Mungu.

740 Kwa hivyo mwaona hapo, mawe haya yaliyotumwa wakati huo, ya Ufunuo hapa, ni yale—yale mawe yalikuwa zawadi walizopelekeana wao kwa wao. Ambayo yaonyesha tu. . . Biblia ilisema, Ufunuo hapa, ilisema, "Yeye aliye na akili na aihesabu

hesabu ya mnyama huyo. Yeye aliye na akili afanye *hiki na kile*. Na yeye aliye na roho ya karama fulani afanye *hiki na kile*." Mwaona jinsi kanisa lilivyopungufu?

741 Kijana mmoja aliniuliza asubuhi hii kuhusu karama za roho, kuhusu kunena kwa lugha. Kijana, mwaminifu sana, naamini yeye atakuwa mhudumu hivi karibuni. Na kuhusu kanisa, nilisema, "Kunayo mengi sana yaliyo ya kimwili. Hatuyataki hayo, lakini twataka jambo halisi. Tunalionea shauku."

742 Huwezi kuyafundisha kanisani; muda si muda, unapata, mmoja ana lugha, mmoja ana zaburi, ndipo huna budi upiganie kuondosha kile kitu. Lakini Mungu anapotoa karama kwa uweza Wake mkuu, itajidhihirisha yenyewe. Naam. Ona, hizo karama za Mungu, hizo ndizo anozolitumia Kanisa lipate kushinda.

743 Sasa, mpinga Kristo ana mazuri na mabaya, ana njia—njia iliyopotoshwa ya kufanya hivyo. Na hiyo ni Milki ya Kirumi ambayo hupelekeana zawadi wao kwa wao, zawadi za kawaida. Mungu huwapelekea washindi zawadi za roho; Warumi hupelekeana zawadi za kawaida wao kwa wao.

744 Twaamini Roho Mtakatifu ni Roho, twampokea kwa ubatizo utokao Juu.

745 Kanisa Katoliki hufundisha, "Eukaristi takatifu ambayo ni mwili wa Kristo; kuwa upokeapo mkate huu na ule mkate mwembamba ulioviringika, ni Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu, eukaristi takatifu." Ona?

746 Twaamini ni kipande cha mkate, hatuamini ni mwili wa Kristo, (tunajitayarisha kuupokea katika dakika chache). Twaamini unawakilisha ule mwili wa Kristo. Lakini si . . .

747 Hiyo ndiyo tofauti kati ya fundisho la Katoliki na la Protestestanti. Ona? Kanisa Katoliki husema, "Mwili ule ni" . . . Mkate ule *ni* mwili hasa. Kanisa lina mamlaka ya kuugeuza huu." Je, mmepata kuona Mkatoliki apitapo karibu na kanisa huinamisha kichwa chake, na kufanya alama ya misalaba? Ni kwa sababu hiyo taa dogo inawaka kanisani pale chini ya kile chumba kidogo. Kina taa ndogo pale, na huo mkate mwembamba wa mviringo uko humo. "Nao huo ni mwili wa Kristo." Na upokeapo huo, bila shaka unapokea mwili halisi wa Kristo katika ushirika wako wa kwanza na maungamo yako na kadhalika. Unapokea ule mwili halisi wa Kristo.

748 Twasema kuwa *unawakilisha* mwili wa Kristo, ona, kuwa kile si kitu kingine ila kipande cha mkate. Na haijalishi kama ingalikuwa hata si mkate, kama ingelikuwa kitu kingine cho chote, ingekuwa tu kuwakilisha vile vile. Vivyo—vivyo hivyo hasa. Hata wao . . .

749 Kama watu hawa wasemao, "Singebatizwa kwenye bwawa, nataka nibatizwe mtoni."

750 Kuna tofauti gani, mradi tu umebatizwa? Kama ni katika bwawa, na. . .Naam, Filipo alibatiza katika bwawa. . .yule towashi alipobatizwa. Filipo alipombatiza yule towashi bwawani, Roho Mtakatifu alimnyakua hata Yeye akamtwaa Filipo, yeye hakuonekana kwa maili mia mbili. Alitwaliwa katika Roho, akapewa gari—gari moja kwa moja toka Mbinguni kwa maili mia mbili. Amina. Ajabu!

Sasa:

> **Watakatifu watakuwa wapi baada ya ule utawala wa miaka elfu moja? Nao watakuwa na miili ya aina gani?** Nitarudia hilo katika muda wa dakika chache [Ndugu Branham ajibu hili mwanzoni mwa aya ya 820, kama swalila 74—Mh.] Watakuwa pamoja na Yesu.

751 Vema, swa—swali la saba:

72. Tutahukumuje malaika?

752 Hilo lapatikana katika. . .Tutahukumuje malaika? Kwa kuwa sisi tu wana wa kiume na wa kike wa Mungu. Malaika ni watumishi; sisi tu wana wa kiume na wa kike wa Mungu. Na Biblia ilisema kuwa tutawahukumu malaika Naam. Sasa, sasa kama mta. . .

Swali la 8:

73. Kwani nywele kwa ajili ya malaika wa I Wakorintho?

753 Sasa mtu fulani anifungulie 1 Wakorintho, ile—ile sura ya 11, nasi tutaona hapo, na utatambua kuwa ile—ile. . .Katika I Wakorintho, ile—ile ya 11, tutaona kwamba Paulo ananena. Hebu nifangue kwa dakika moja hivi ndiposa tutaisoma upesi sana kisha tuta—tutalijibu.

754 Nina jambo la kusema kuhusu kifungu hiki kingine hapa ambacho natumaini Bwana atatupa jinsi itupasavyo kujua. Kama mtu ye yote amekipata. . .Nadhani hiyo ni sura ya 11, naam, vema. Sasa sikilizeni kwa makini, kwa makini sana sasa, ili mfahamu. Sasa chukua dhamiri yako yote na uiweke mfukoni mwa fulana yako hata nitakaposoma hili, mwaona, kuifafanua. Sikiza, kwa makini sana, hili ni BWANA ASEMA HIVI.

> *Mnifuate mimi kama mimi nilivyo. . .wa Kristo.* (Paulo alisema, "Mnifuate kama mimi ninavyomfuata Kristo.")
>
> *Basi nawasifu, kwa sababu mmenikumbuka katika mambo yote, nanyi mmeyashika yale mapokeo vile vile kama niliwa. . .nilivyowatolea.*
>
> *Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu.*

755 Mwaona jinsi ilivyo? Mungu, Kristo, mwanamume, mwanamke. Sasa.

> *Kila mwanamume, asalipo, au anapohutubu, naye amefunikwa kichwa,* yuaaibisha Kristo.
>
> *Bali kila mwanamke asalipo anapohutubu, bila kufunika kichwa chake—*yuaaibisha *kichwa chake;*. . .

756 Sasa tutaona kwa dakika moja nivi, na kuwaonyesha ninyi kuwa nywele kwa mwanamke ndicho kifuniko chake;

> . . .*kwa maana*. . .*ni sawasawa na yule aliyenyolewa.* (maana yake ni kwamba kama—kama atakata nywele zake, basi zikatwe zote)
>
> *Maana mwanamke asipofunikwa na akatwe nywele:* (akatwe maana yake ni anyolewe, ona). . .*au ikiwa ni aibu mwanamke kukatwa nywele zake, au kunyelewa, na afunikwe.*

757 Sasa tunaliendea moja kwa moja swali hili hapa unapouliza. Ona? Vema, sasa ni kosa kwa mwa—mwanamke kukata nywele zake kulingana na Biblia. Sasa sikiza papa hapa uone kama Biblia haimpi mwanamume haki ya kumtaliki mkewe akikata nywele zake, ona kama hili ni sahihi au la.

> *Mwanamume aki*. . .*Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa* (hiyo ni kuwa na nywele ndefu), *Kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume.* (je, uliwahi kuwaza hilo?)

758 Sasa nataka kukoma hapa, kwa kuwa nataka hili liingie ndani kabisa, ona. Na sasa kumbuka, nimeona makumi ya maelfu ya wanawake (nawajua hivi sasa, na wengine wao wameketi katika kanisa hili) walio na nywele fupi, walio Wakristo. Na kile ninachowalaumia si ninyi, ni jinsi mmefundishwa. Ona? Naam. Mhubiri wenu hajapata kuwaambieni hili. Lakini kama ye yote wa wanawake wa Maskani haya wako hivyo, basi ana hatia. Ona, kwa kuwa hakika sisi huwaonya.

759 Sasa, sasa tazama hili:

> . . .*mwanamume*. . .*Kwa maana*. . .(kifungu cha 7). . .*Kwa maana mwanamume*. . .

760 Sasa, nani anayenena hapa? Sasa, wakati mwingine mwanamke asema, "Ee, maskini Paulo alikuwa mchukia wanawake."

761 Vema, sasa hali tuko kwa hilo, hebu tufungue hapa kwa Wagalatia 1:8, na tuone yale Paulo asema kuhusu hilo. Ona, katika Wagalatia 1:8, tutaona kuwa Paulo alisema hapa katika Wagalatia l:8:

> . . .*ijapokuwa sisi au Malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote* isipokuwa hii mmekwisha kuisikia *na alaaniwe.*

762 Sasa msinilaumu, mmlaumu Yeye, ona.

Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume.

763 Sasa chunguza kifungu kinachofuata:

Maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume;

Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamuke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume.

764 Sasa, nakusudia hili sasa kwa upendo halisi na wema, nami natumai mwafahamu hili jinsi nisemavyo. Lakini Amerika... Kama mtu asafiriye dunia nzima, Amerika ina baadhi ya sheria za wanawake wao zilizo duni sana, na potovu kuliko taifa lo lote ulimwenguni. Paris, Ufaransa, ingekuwa orofa ya angani kama si jinsi Amerika iachiliavyo wanawake wake kufanya. Ni aibu!

765 Je, mnajua kuwa mungu wa Amerika ni mwanamke? Naweza kuthibitisha hilo kwa Biblia hii. Naam. Je, watambua kuwa halina budi kuwa hivyo ili kanisa Katoliki lipate kuingiza fundisho lao la bikira Mariamu?

766 Sasa, kama mwanamke aliumbwa si kwa ajili ya mwanamume si...Kama mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke akaumbwa kwa ajili ya mwanamume, basi mtamwabuduje mwanamke? Ona? Sasa, kilichoisababisha, ilianzia Paris na kutua Hollywood. Sasa Paris haina budi kuja Hollywood kupata mapambo yao na kupata mitindo yao na kadhalika, ni udhilifu wa wanawake wetu wa Amerika.

767 Ni nini? Taifa letu limefifia sana hata wamechukua kazi toka kwa wanaume, na kuweka wanawake nje pale katika mahali hapa, hadi asili mia tisini, karibu hao, ni malaya. Naam, nena kuhusu wanaume kupungukiwa, kwa kuwa wamewapa wanawake kazi zao. Nao wamekuwa wanyonge sana hata wakawaweka wanawake kama maafisa wa usalama kwenye barabara za mji. Hiyo ni aibu kwa taifa lo lote! Naam bwana. Utafanya nini kwake?

768 "Unafanyaje kwake, Ndugu Branham?" Yanibidi niliheshimu, mimi ni raia wa Amerika, natenda yale bwana mkubwa asemayo yafanywe. Kama niliwahi...Kama—kama jamaa imepoteza heshima yake kwa jamaa (watoto kutowaheshimu wazazi), jamaa hiyo imevunjika-vunjika vipande. Kama—kama kanisa halimheshimu mchungaji wake, naam, kanisa hilo limepotea. Na kama taifa lisipoheshimu mahakama makuu na uamuzi wake, taifa hilo limevunjika-vunjika vipande. Ndivyo hasa. Hatuna budi kuheshimu mambo

hayo kwa maana hao ndio bwana wakubwa, ona. Lakini si halali tangu mwanzo. Hakika!

769 Je, mlitambua kuwa mwanamume katika Biblia . . . katika Mwanzo, sura ya 1, Mungu alipomuumba mwanamke na—na mwanamume, na kumfanya mwanamume na mwanamke, na Mungu, akamwambia Hawa kuwa "mume wako atakutawala, atakuwa mtawala wako"? Nena hilo katika Amerika na uone ambapo utafika! Wee, sivyo, wanawake wanatawala wanaume; hawana budi kufanya hayo, umeidhinishwa . . .

770 Ningeleta wanawake, kama ingenibidi, toka chumbani mwangu pale, kwa madazan, waadilifu . . . Sisemi wanawake wote lazima wasifanye kazi wakati mwingine; labda wana mume aliye mgojwa au cho chote kile, nao hawana budi kufanya kazi. Lakini isipowalazimu, yafaa wasifanye. Mahali pao ni nyumbani, ngome yao ndogo, hapo ndipo hasa iwapasapo kuwa.

771 Na wanawake wetu wa Amerika wamejaliwa kufanya wapendavyo. Hata katika wanyama wote na kadhalika, kitu hicho kinapochukua mamlaka, inatendeka na kuaibisha jamii yote.

772 Kuna ndege mdogo wa kike Afrika, naye ni ndege mwenye umbo nzuri sana.

773 Sasa kwa kawaida, wa kike ndiye mwenye umbo baya sana kati ya hao wawili. Ndume kila mara ndiye mzuri sana, paa dume, kulungu dume, tausi wa kiume, ji—jimbi, na kila mara walio . . . Kwa sababu, wa kike ni ndege wa nyumbani. Yeye hukaa kwenye kiota, huwalea makinda yake. Anageuza umbo lake kwa ajili ya mwewe, nyoka, na mbwa mwitu, na wengineo, ona, kuwalea makinda yake.

774 Lakini katika jamaa ambapo . . . au katika hali ambapo—ambapo mwanamke, au jike, hushinda katika urembo, kila mara ni kitu kipotovu. Katika Afrika, chukua ndege . . . Kuna ndege mdogo kule ndiye wa pekee nimjuaye barani, ambapo wa kike ni mrembo kuliko wa kiume. Na iwapo . . . Ndege huyo—huyo ni kahaba daima. Atakimbia hapa na pale na apate mwenziwe, na akimbie nje na atage kundi la mayai baada ya kujuana na mmoja, na kuacha wa kiume akiyatamia hayo mayai aenda kupata mwenziwe mwingine. Hiyo ni kweli hasa. Ona? Mnaona ninalokusudia?

775 Ina . . . Sasa tazama katika Amerika siku hizi, wanawake wetu. Kijana mwanamume toka Kentucky aliniambia, siku chache zilizopita, ya kwamba kulikuwa na wanawake mia nane kule wakifanya kazi kwa kiwanda fulani hapa Kentucy. Naye akasema, "Nimgejisikia huru kuapa ya kwamba mia nne wao bila shaka ni makahaba mjini, na ni wanawake walioolewa na wana watoto." Mtu mmoja alimchukua mke wake pale na kumpiga sana kwa ubao, nusura amuue. Na mwingine alimpiga

mwanamme fulani risasi. Na mwingine akakatana na kupigana. Hilo halipaswi kutendeka. Hilo si sahihi.

776 Rudisheni mwanamke jikoni panapompasa, ndipo kila kitu kitakuwa shwari. Lakini mnapomweka kule nje katika kazi za umma, amepotea. Hakika . . . sisemi kuwa . . .

777 Wanawake wa Amerika huinua mapua yao na kusema, "Hakuna cha Hiyo." Na, "Nionyeshe." Bila shaka, yakubidi kufanya hivyo, kwa sababu Biblia ilitabiri mngefanya hivyo. Hamna budi kulitenda.

778 Na hapa wakati . . . Ilikuwa muda mwingi uliopita, katika kanisa Methodisti, mwanamke angalikata nywele zake, angelifukuzwa kanisani. Bila shaka, walifanya hivyo. Naam, hakika. Wanazarine, Pilgrim Holiness, Wapentekoste, hao wote walikuwa wakifanya hivyo. Imekuwaje?

779 Mwajua sababu? Mna vijidada fulani mle mimbarani. Naam hasa. Mtu fulani anaogopa riziki zao . . . wanaogopa mngewatenga, mngewafukuza kanisani. Hawathubutu kule kusimama, kusimama kwa Neno la Mungu au laumiza au haliumizi. Naam, hasa.

780 Sikiza hapa, mwanamume ndiye mtawala, usidhani unaweza kutawala nyumbani. Wewe si mtawala nyumbani. Wewe hakika . . . Naam, si mtumwa sasa, lakini u msaidizi. Na Adamu . . . Mwanamume ana mamlaka juu ya mkewe, mkewe ni daraka lake peke yake. Mungu hufanya matendo ya mwanamke kuwa juu ya mumewe. Sasa, soma na uone kama Mungu hasemi hayo sasa.

> *Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunika kichwa, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu . . .*

781 Mungu si mwanamke, Mungu ni mwanamume. Mwajua wanampofanya bikira Mariamu na kadhalika, na kuombea . . . au uombezi na kadhalika, na kumwomba bikira Mariamu, mwajua hilo lanikumbuksha mimi nini? Yule mungu mkuu wa kike, Diana, ambaye Paulo alimkeamea na kumwondosha. Naam, Yeye alisema, "Naam, Mungu si mwanamke:."

782 Jiwe lilianguka shambani, nao wakasema miungu ilitupa chini sanamu yao, hiyo ndiyo sababu wanawake wa kule Korintho, na juu mle ndani, hao . . . waliomwabudu Diana, walitaka kuwa wahubiri.

783 Hao walisema, "Hasha, roho alitwambia tungehubiri."

784 Yeye akasema, "Au je? Neno la Mungu lilitoka kwenu? au kuwafikia ninyi peke yenu? Mtu akijidhania mwenyewe kuwa wa rohoni au nabii, na ayakubali yale ninayoyasema ni amri ya Bwana: wanawake na wawe kimya na watiifu kanisani, wasifundishe wala kuwa na mamlaka yo yote." Ndivyo ilivyo hakika. Hivyo ndivyo Maandiko yalisema. Ona? Na Mungu

ataweka hayo juu ya kundi la wahubiri kwenye Siku ya Hukumu.

785 Vema, sikiza! Unasema, "Vema, nawaambieni, nilifundishwa hilo." Wajua ikupasavyo sasa! Naam. Kama wewe au mtu fulani anaanza kunywa dawa, na mtu mwingine akwambie ni sumu, nawe—nawe uinywe haidhuru, hilo ni kosa lako mwenyewe baada ya hayo. Ona?

786 Sasa sikiza hili:

> *Maana mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume.*
>
> *Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani, kwa ajili ya malaika.*

787 Ye yote wenu anayesoma? I Wakorintho, sura ya 11 na kufungu cha 10. Mkichunguza, "mamlaka, mamlaka ya malaika," 1 Wakoritho, kwa kuwa malaika ni binadamu, mjumbe. Tazama, ni herufu ndogo tena ya "m." Ambapo Malaika wanahusika, Malaika wa Mbinguni, ni "M" kubwa, herufi kubwa ya "M." Mnamo "m" ndogo ni malaika wanadamu.

> *Walakini si mwanamume pasipo. . .au mwanamke,. . .walakini si mwanamke pasipo mwanamume— mwanamume, katika Bwana.*
>
> *Maana kama mwanamke alitoka katika mwanamume, vile vile mwanamume naye huzaliwa na mwanamke,. . . na vitu vyote asili yake hutoka kwa Mungu.*
>
> *Hukumuni. . .ninyi wenyewe katika nafsi zenu. Je! inapendeza mwanamke amwombe Mungu* (akiwa na nywele fupi) *asipofunikwa kichwa?* (waza hilo sasa)

788 Sasa tazama:

> *Je: hayo maumbile yenyewe hayawafundishi ya kwamba mwanamume akiwa na nywele ndefu,. . .*

789 Kwa hivyo inahusu nini? Nywele: Hamwoni kile Paulo ananena? Nywele, nywele ndefu:. . .Mwanamke apaswa kuwa na nywele ndefu. Kifungu cha 14 sasa:

> *Je! hayo maumbile yenyewe hayawafundishi ya kwamba mwanamume akiwa na nywele ndefu ni aibu kwake?*

790 Mwafahamu? Ni aibu kwa mwanamume kuwa na nywele ndefu, lakini mwanamke. . .hapo ni mahali pa mwanamke. Mungu alimuumba mwanamume tofauti na mwanamke, jinsia na maumbile na cho chote kile. Hapaswi kuvalia mavazi. . . Biblia ilisema kuwa "Mwanamke akivaa suruali ndefu wala vazi lo lote limpasalo mwanamume, ni chukizo na uchafu na najisi machoni pa Mungu." Na Mungu atamwadhibia hilo. Mtamsikiza nani? Lakini hii ni Biblia:

791 Unakimbia hapa na pale na kusema, “Naam, nadhani ni vizuri kwa . . . kuona wanawake wamevalia suruali ndefu.” Lakini Mungu aliwaumba tofauti, Yeye awataka wao wavalie tofauti.

792 Biblia ilisema, “Mwanamke akivaa vazi limpasalo mwanamume, ni chukizo.” Mwajua *chukizo* ni nini? Ni kitu kilicho kichafu machoni pa Mungu.” Na Yehova Mkuu awatazamaye kama kitu kiovu . . . Na Biblia ilisema . . .

793 Nanyi mlisema . . . Baadhi yenu wanawake sasa, kwa wasichana wenu matineja, miaka kumi na minane, ishirini, kuwaruhusu wakimbie nje hapa wamevalia hivyo!

794 Nanyi, pia kina mama! Ona? Uendapo nje pale na kuvalia suruali ndefu hizo na vinginevyo na kuishi . . . kutembea katika barabara za mji na—na uvae maskini nguo hizo zilizo uchi sana siku hizi, na kukufanya uonekane kama kitu fulani usicho. Ona? Na kwenda nje kule kwenye barabara za mji ukionekana kisinifu kabisa, huenda ukawa asiye na hatia na mwadilifu mbele ya mumeo na kila kitu, lakini ukienda nje kwenye barabara za mji na mwanamume akutazame kwa kuwa ulijionyesha hivyo, una hatia, na utahukumiwa Siku ya Hukumu kwa ajili ya kutenda uasherati pamoja na kila mwanamume aliyekutazama ulipokuwa hivyo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema.

795 Biblia ilisema, “Mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake,” na una hatia na uta . . .

796 Utakuja hukumuni na kusema, “Bwana, wajua moyo wangu; nami sikupata kutenda uasherati, nalidumu mwaminifu kwa mume wangu.”

797 Lakini hapa kutakuwako mwanamume, kutakuwako mwingine, hapa mwingine, mwingine, kumi na tano, ishirini, thelathini, arobaini yao wamesimama pale wakisema, “Una hatia ya uasherati!” Mbona? Baadhi ya wanaume walikutazama.

798 “Vema, sikuhusika kwa vyo vyote vile.” Vema, mbona ujionyesha mwenyewe hivyo? Hali Mungu alikwambia usiyavae, ni chukizo kufanya hivyo, na unaenda kusikiza kipindi cha *Je, Ni nani Ampendaye Susie?* Au cho chote kile . . .

799 Je, ulitambua kile kilichotendeka kwa mume wa *Je, Ni Nani Ampendaye Mme wa Suzie?* Nyote mliona hayo hapa hivi majuzi gazetini. Tulipokuwa kule Casper, Wyoming, ikatukia. Na jina lake ni nani? Mwanamume huyo . . . kwa kile kupindi cha *Twampenda Susie,* au kile kilikuwa—hicho kilikuwa nini jamani? Ile . . . Naam, kile ambacho ninyi nyote hukaa nyumbani Jumatano usiku na kukosa kuhudhuria mkutano wa maombi ili mkitazame. Hicho ni nini sasa? Twampenda . . . Jina la hicho ni nini? [Dada fulani asema, *“Nampenda Lucy”*—Mh.] *Nampenda Lucy*, mumewe anasemekana ana . . . anazurura-zurura, amelemewa kule Reno, Nevada, akiwa na msichana

mweusi, amekuwa akiishi naye kwa miaka mingi. Na hayo ndiyo mkaayo nyumbani kuona badala ya kwenda kusikiza Injili. Mwanamke huyo aliyaungama. Ee, rehema! Hakuna cho chote kisafi nje ya Yesu Kristo.

800 Tahamaki, ndugu, nita—nitawaambia ninyi—ninyi wanaume, baadhi ya wale...Mwasema, "Ee, lo, tazama waungwana." Baadhi ya—koho waovu sana tulio nao, kipanga, ni ndege malidadi. Huwezi kumfahamu ndege kwa manyoya yake, ona. Kwa hivyo kumbuka tu hilo. Jamani!

801 Sasa tazama:

> *Je: hayo maumbile*...(hicho ni kifungu cha 14)... *yenyewe hayawafundishi ya kwamba mwanamume akiwa na nywele ndefu ni aibu kwake?* (hiyo ni ya mwanamke)
>
> *Lakini mwanamke akiwa na nywele ndefu ni fahari kwake*...

802 Sasa yeye ananena kuhusu nini? Kofia ile ninyi Wakatoliki huvaa kanisani? La, hakika! Kifuniko kidogo juu ya vichwa vyenu pamoja na vitambaa vyenu? Yeye ananena kuhusu nywele zenu!

803 Sasa: Na mwanamke anapokata nywele zake huondoa utukufu wake, na haruhusiwi mimbarani kuomba, wewe... kile ilichosema hapa. "Je ni jambo la kawaida kwa mwanamke kuomba asipofunikwa kichwa chake?" Kasema hapa, kasema, "Vema hana budi kukata nywele zake." Kwa hivyo na anyolewe kabisa. "Na akinyolewa kabisa," kasema, "ni fedheha, ni aibu kwa mwanamke kufanya hilo." Ndipo akasema, "Yeye apaswa kufunikwa." Sasa, nina—ninasoma tu waraka wa Paulo. Ninyi nyote, ni juu yenu kuona.

> *Lakini mwanamke akiwa na nywele ndefu ni fahari kwake. Kwa sababu amepewa zile nywele ndefu ziwe badala ya mavazi.*

804 Je, ilisema angepewa kofia? Ninyi Wakatoliki au ninyi Waprotestanti, nyote wawili mnaoenda kanisani na hupenda kuvalia kofia, kasema, "Vema, naenda kanisani, yanipasa kuvaa kofia." La, yakubidi uache nywele zikue. Hiyo ndiyo tofauti: Ona?

> ...*kwa sababu amepewa zile nywele ndefu ili ziwe badala ya mavazi.* (na ni aibu kwake kuja kanisani bila kufunikwa, kwenda madhabahuni kuomba)
>
> *Lakini mtu ye yote akitaka kuleta—kuleta*...(siamini naweza kutamka neno hilo, f—i—t—i—...)...*Fitina—fitina* (mwajua fitina ni nini?)*, sisi hatuna desturi kama hiyo, wala* Kanisa *la Mungu.*

805 Sasa, mkitaka kubishania nayo, bishaneni na Hilo. Vema, unataka kuleta fitina, "Ee, hamna tofauti yo yote. Na tuwaachile

waendelee. Mbona, nadhani si kitu. Ni. . . si vile nywele ilivyo, haidhuru, ni jinsi moyo ulivyo." Hilo ni kweli; kama moyo u safi, nywele itakuwa safi (uhu-uhu).

806 Endelea, unataka fitina, Paulo alisema, "Hatuna desturi kama hiyo, wala Kanisa la Mungu." Kasema, "Ukitaka uwe upande wa Kaini, vema, endelea tu." Lakini haya ndiyo Paulo alikuwa akisema.

807 Ee, nami sitaki kucheka, kwa kuwa si jambo la kuchekelea. Lakini nawaambieni marafiki, ni aibu kuona jinsi mambo haya yameruhusiwa kutendeka. Ni . . .

808 Sikiza! Kwenu, dada zangu wapendwa, nataka mwonekane wazuri sana na muwe wazuri sana, hivyo ndivyo iwapasavyo kuwa kuwa. Hivyo ndivyo iwapasavyo kuwa. Nanyi yapasa muwe wazuri na wachangamfu na kadhalika kama mwezavyo waume wenu wanapokuja, vivyo hivyo kama angalikuwa mpenzi wako. Na inakupasa kumlaki mlangoni na—na busu tamu tu kama ilivyokuwa siku uliyombusu madhabahuni awe mume wako. Naam. Sikulaumu kwa kuonekana mrembo sana na kuwa mrembo. Nami nakutaka uwe hivyo, Mungu ajua nataka hivyo.

809 Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa nikiongea na Jack Schille. Nani amemsikia Jack Schiller? Mhubiri mashuhuri sana Methodisti iliyo naye. Yeye alisema, "Mwanamke fulani alikuja na kusema . . . nywele yote chafu, huku akitafunatafuna peremende, na karibu uchi, akisema, "Mwajua, mume wangu hata hanitaki."

810 Yeye akasema, "Simlaumu."

811 Naam, basi. Lakini kile unachohitaji kufanya yakupasa ukifanye sawa. Usichukue uchangamfu wako na urembo toka Hollywood, utoe katika Biblia. Mbele za Mungu: kuwa bibi, tenda kama bibi, valia kama bibi, kuwa msafi. Tenda kama bibi, usivalie hizo . . .

812 Mwanamume ye yote anayemruhusu mkewe kutoka nje na kuvaa vitu hivyo viovu mbele ya watu, na hivyo vitu viovu . . . kuenda uwanjani na kukata nyasi, na kadhalika, bwana, nakwambaia ndugu! Si—sikusudii kuwa mchoyo, ni . . . Mungu ajua moyo wangu. Lakini itanibidi ku . . . itanibidi kufanya mabadiliko chungu nzima kabla nimemruhusu wangu kufanya hivyo. Nitakuwa mtawala kilimani kule mradi tu niwezavyo, mwaona; na nitakaposhindwa, nitaondoka. Naam.

813 Ee, ndugu, hiyo ni aibu na fedheha kwa wanawake kufanya hivyo. Nami—sikusudii, dada . . . si—siwaaibishi ninyi, najaribu kusema . . . Kanisa letu hapa halina wafuasi, watu huja tu hapa. Lakini hii ni nyumba ya Mungu, nasi bila shaka huwaambia watu wasivalie vitu hivyo. Ni . . . utatoa hesabu yake kwenye Siku ya Hukumu. Sasa tazama hapa. Na acheni nywele zenu zikue, ona, na muwe mabibi.

814 Basi:

> *Lakini katika kuagiza haya...siwasifu ya kwamba mnakuanyika...si kwa faida bali kwa hasara.*
>
> *Kwa maana kwanza mkutanikapo kanisani nasikia kuna faraka kwenu, na mengineyo*...(inaendelea sasa kwenye meza ya ushirika)

815 Sasa sikiza hilo. Hiyo ndiyo sababu malaika...

816 Sasa Ndugu Palmer, sikwambii kwa tepe hii, unahubiri mambo yale yale kule ambayo nahubiri hapa. Lakini wajua vizuri sana, na wewe kama mhubiri, wajua hayo ni Kweli, ndugu. Vema.

817 Kwa hivyo *malaika* hapa ni "mwanadamu." Ukichunguza, Ndugu Palmer, ni herufi ndogo, "malaika." Na Biblia yaendelea. Yeye ananena kuhusu mume na mke wake, ona, hilo ndilo linalonenwa.

818 Hivyo ndivyo watu huhangaishwa na Biblia, wao husema "Vema, Mungu anasema jambo moja *hapa*, na lingine..." Sivyo, hu—hujui unechonena. Shikilia yanayonenwa, hivyo, tu. Yeye ananena kuhusu mwanamume na mwanamke.

819 Sasa kitu kimoja zaidi ninachotaka kugusia kabla hatujamaliza, kitanichukua dakika mbili hivi:

74. Watakatifu watakuwa wapi baada ya ile miaka elfu? Nao watakuwa na mwili wa aina gani?

820 Nafikiri hili ndilo swali tamu sana, napenda tu hilo. Sasa hebu tulichunguze moja kwa moja.

821 Hapo mwanzo, Mungu...Tutarudi tena kwa mafundisho yetu ya Waebrania kwa dakika chache. Mungu alikuwa hiki kisima kikubwa mno chenye rangi saba. Wangapi wajua hilo? Ona? Na wangapi wajua kuwa Mungu ana Roho saba? Hakika, Roho saba. Naye yule mwana-kondoo alikuwa na macho saba, kadhalika, hayo yote yanakuja pamoja sasa. Ona? Sasa, huyo alikuwa Mungu.

822 Sasa wakati Yeye (yule Logos) alipotoka kwa Mungu, ambayo ilikuwa Mungu akitoka kwa hiki kisima kimoja kikuu kuingia mwilini katika mfano wa—wa mwanadamu, nayo ikafanya Logos, ambayo tunaiita mwili wa Kiungu.

823 Sasa, ukichukua ule mwili wa Kiungu unapoutazama huo, ni mwanadamu. Sasa kwa kuwa tuna...Sasa, hapo ndipo tulipokuwa hapo mwanzo sasa. Sasa, hamwelewi hilo sasa, lakini mlikuwa kule nyuma mwanzoni hivyo. Mwanadamu alipoumba...Mungu alipomuumba mwanadamu katika mfano Wake, Yeye alimfanya katika mwili wa Kiungu. Na yeye alimweka tu ndani ya mwili...Mungu alipomuumba mwanadamu katika mfano Wake, katika sura Yake, walikuwa...Katika Mwanzo 2, kulikuwako...au

Mwanzo 1:28 naamini ndipo, "Wala hapana mtu wa kuilima ardhi," na Mungu alikuwa amekwisha kuumba mwanamume na mwanamke. Naam, "Hapana mtu wa kuilima ardhi."

824 Ndipo Mungu akamshusha mwanadamu kidogo zaidi na kumweka katika uhai wa mnyama, hiyo ni mwili huu, kama tu wanyama kusudi ailime ardhi, angegusa. Huo mwili wa Kiungu haugusi, hauoni, haunusi, hausikii, hizi hisi tulizo nazo. Kwa hivyo Mungu alimweka mwanadamu chini pale ili—ili apate kugusa na kusikia.

825 Na—na alipotembea katika Bustani ya Edeni, kwanza kama mwili wa Kiungu, (kama Roho Mtakatifu alivyo ndani humu sasa akitembea ndani humu), aliishi maisha ya wanyama. Alitawala kila kitu, lakini hangelima, ona. Kwa hivyo Mungu alimweka yeye katika mwili huu apate kuilima ardhi. Akampa hisi zake tano, kuilima ardhi na kulima sha—shamba la mizabibu na—na kadhalika, hata hivyo mwanadamu angali alionekana mpweke. Ee, huu ni mfano mzuri sana.

826 Tazama, kwa kuwa yeye alipoumbwa kwanza, aliwaumba watu wawili, pamoja. Aliumbwa mwanamume na mwanamke, huyo mtu alikuwa hivyo. Biblia ilisema alikuwa hivyo. Mungu alimuumba mtu akiwa mwanamume na mwanamke pia, "alimuumba." Tazama sasa, mtu alipotenganishwa na ule mwili wa Kiungu na kuwekwa katika mwili, yeye alikuwa—hakuwa pale kabisa; sehemu yake ilikuwa ingali ule mwili wa Kiungu, kwa hivyo haikuonekana sawa.

827 Akaondoka ng'ombe wa kiume na wa kike, akaondoka farasi, na akaondoka ndama, na kadhalika, wawili—wawili. Lakini Adamu, yeye . . . ilikuwa . . . Ona, kulikuwa na kasoro fulani. Shauku iyo hiyo ilionyesha kuwa kuna mwenziwe anayemngoja. Mwafahamu? Na mawazo kwamba hatuna budi kufa hapa, ya kwamba tunasumbuka na kuhangaika, nasi tunatumainia Uzima ambao hauna kifo, inaonyesha unatungoja sisi. Ona?

828 Naye Adamu alikuwa peke yake. Na Mungu, kuonyesha kuwa hawangetenganishwa . . . Sasa naenda kurudia jambo lili hili, kwa dakika moja.

829 Tazama, Yeye hakwenda na kupata matope na kumuumba Hawa, lakini Yeye alimuumba toka kwa matope ya asili, Adamu. Akatwaa ubavu kati ya mbavu zake na kumfanyia msaidizi, na huyo alikuwa Hawa. Yeye aliumbwa kwa ajili ya mwanamume, na sehemu ya mwanamume. Hawa alikuwa sehemu ya Adamu mwanzoni, katika uumbaji, katika mwili wa Kiungu. Alikuwa sehemu yake hapa katika uumbaji. Yeye hangetenganishwa katika uumbaji mwingine, ilimpasa kuumbwa katika uumbaji ule ule.

830 Hiyo hasa ndivyo sababu Kristo na Mungu iliwapasa kuwa Nafsi ile ile, haingekuwa vinginevyo. Kama Yeye angekuwa

mtu mzuri au nabii, Yeye hangekuwa Mkombozi, ilimbidi kuwa Muumba Mwenyewe. Bali Yeye yungali katika ule mwili wa Kiungu sasa, mwaona, na jinsi Yeye alivyokuwa wakati huo.

831 Sasa mtu fulani alikuja chini hapa na yeye—yeye alikuwa wa ajabu na Mungu alipenda hilo. Yeye alisema, "Vyema, na wakae duniani na waishi mle milele. Hivyo tu; Mi—Milele, na kadhalika na kadhalika na kadhalika. Na ikue tu, na kila mmea uzae, na kadhalika. Na mwanadamu aishi, na wanyama waishi, na kadhalika, milele na milele. Naam." Ona?

832 Ndiposa dhambi ikaingia. Nami nataka kusema jambo hili. Katika . . . Watu wengi hufanya kosa sana kwenye Andiko hili moja, na hiyo ni Zaburi 23. Wao huisoma hivi, "Naam, nijapopita katika bonde *jeusi* la uvuli wa mauti." Sasa hamna kitu kama hicho. Biblia haisemi, kuwa, "Uvuli mweusi wa bonde . . . bonde jeusi la vivuli vya mauti."

833 Yasema, "Nijapopita katika bonde la uvuli wa mauti." Sasa, isijakuwa uvuli haina budi kuwa na nuru ya kutoa kivuli hicho. Ona, Daudi, akiwa nabii chini ya upako, yeye hakufanya kosa; yeye alisema kweli tu. "Naam, ninjapo . . . " (si kutembea katika bonde *jeusi)* "lakini nijapopitia katika bonde la *vivuli* vya mauti."

834 Ndipo yakubidi uwe na asili mia fulani ya nuru kusudi upate kivuli. Na hivyo ndivyo ilivyo hapa. Sisi sote tu wa kawaida na wa kimbinguni. Mwili huu hauna budi kufa, na ulizaliwa na mwanamke; si bure bali kwa . . . Si kuzaliwa na Mungu, wewe umetoka kwa Adamu na Hawa. Uwe mweusi, mweupe, au ye yote yule, wewe u mzao, ukoo wa Adamu na Hawa. Hilo laufanya mwili wako "uliozaliwa katika dhambi, ukaumbika katika maovu, ukaja ulimwenguni ukinena uongo." Umehukumiwa na kupata adhabu mwanzoni mwa maisha yako, si . . . bila hata nafasi.

835 Sasa, kwa kuwa roho ile uliyo nayo ilitokana na maumbile, na maumbile yakaja kwa kujuana kimwili, tamaa ya wanaume na wanawake huzaa watoto wenye asili ya dunia. Na hebu kamwache mtoto huyo pekee, na usimfundishe cho chote sahihi, yeye atakosea. Usimfundishe mazuri wala mabaya, atachagua mabaya. Kwa sababu ni asili yake kufanya hayo.

836 Mtazame maskini mtoto mdogo, mrefu *hivyo*, hupatwa na hasira sana; ata . . . a—atakunja mikono yake, na kuwa mwekundu wa uso, na kapweza pumzi. Hakika. Ni nini? Ni asili yake. Yeye aliipata kwa baba yake au mama yake, mmojawao: alikuwa na hasira kutosha kupigana na msumeno, ama baba yake. Kama sivyo, babu yake au nyanya yake alikuwa nayo. Ona, ni mzao.

837 Kwa hivyo hilo lafanya . . . Unazaliwa duniani. Unakuja kwa asili yako, na utu wako wote u mweusi na wenye moshi, na umehukumiwa, na kulaaniwa na unaelekea kuzimuni. Naam!

838 Bali unapozaliwa mara ya pili, Nuru ya Mungu huiangazia nafsi yako (haleluya) ndipo si tena bonde jeusi bali ni bonde lenye kivuli. Huenda umefunikwa hapa kwa mwili, na vinginevyo usoni mwetu, lakini kuna Nuru ya kutosha ndani mle. Na hivi karibuni Nuru hiyo na giza hilo havina budi kutenganishwa: Na nuru inapoangaza, giza huondoka. Na tuendapo kuwa na Kristo katika mwili huo, giza na mauti hutoweka, nasi tunazukia Nuru kamilifu. Mungu atukuzwe: Naam; hamna tena magonjwa, giza halichanganyiki nayo tena.

839 Hivi sasa tuna magonjwa pamoja na furaha, na tuna afya na nguvu, nasi tuna *vipengee,* na *milima* na *mabonde*, furaha na huzuni na kadhalika. Vema, ni kivuli tu. Tuna mwangaza wa kutosha sasa kujua kuna Nuru pale; nasi tungali katika mwili, katika nyama. Bali hivi karibuni ile Siku itapambazuka. Hapo ndipo yule malaika wa mauti aketipo kwenye liwato la kitanda, hapo ni wakati daktari asemapo yote imekwisha, na hii ya kawaida imeachana na ile ya kimbinguni, nayo nuru imerudi kwenye Nuru, na giza limerudia giza. Ndipo huu mwili ufao utavaa ule usiokufa. Hapo ndipo pale huu uharibikao unapovaa usioharibika. Hapo ndipo huu ufao uanapovaa ule usiokufa, na tunatoka kwenye kiumbe cha wakati kuingia kwenye kiumbe cha Milele. Huwezi kwenda nje pale katika giza tupu, yakubidi uwe na nuru katika giza. Naam. Huo ndio mwili unaopokea.

840 Tunafanyaje? Vema, ndugu yangu mtakatifu, mpendwa dada yangu mtakatifu, mpendwa, kabla dunia haijawekwa misingi, Mungu alipokuumba katika mfano Wake, au kumuumba mwa—mwanamume katika mfano Wake, na kumuumba mwanamke katika mfano wa mwanamume kwa utukufu wa mwanamume, Yeye alikufanyia wewe mwili wa Kiungu. Kama tu Yeye Mwenyewe alivyowaambia 'na tumfanye' wale viumbe ambao aliwaumba, "na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, ule mwili wa Kiungu." Mungu hakuwa amekwisha kuwa mwili bado, Yeye alikuwa katika mwili wa Kiungu.

841 Na Musa alimwona. Musa akalia, "Bwana, hebu nikuone Wewe."

842 Yeye akasema, "Nenda kule ukajifiche mwambani katika majabali. Naye Musa akarudi tena majabalini; na Mungu alipopitia hapo, ule umeme na ngurumo . . . Na Mungu alipopitia hapo, Yeye aliugeuza mgongo Wake *hivi*.

Na Musa alisema, "Ulikuwa ngongo wa mwanadamu." Haluluya!

843 Alikuwa nani? Melkizediki aliyeshuka, yule Mfalme wa Salemu, hana baba wala mama, hana mwanzo wa siku zake wala mwisho wa uhai Wake. Ndiye huyo! Akishuka, huyo ndiye aliyeongea na Ibrahimu. Walimkusanyia Yeye mwili mdogo wa nyama hivyo, na [Ndugu Branham apiga mbinja—Mh.] akaupulizia, akaingia ndani yake, na akashuka na akala ndama,

akanywa maziwa ya ng'ombe, na akala siagi na ugali. Na wale Malaika wawili.

844 Na walipoondoka mle, na vitu hivyo vyote tu [Ndugu Branham apiga mbinja—Mh.] vikatoweka na kutokomea.

845 Sijawahi kufikiria hilo. Hapa hivi majuzi nilipokuwa nikishindilia bunduki risasi, nilikuwa na bunduki.22, ni 220 Swift. Nanyi ndugu mnaotumia bunduki ndani humu mwajua. Hiyo risasi ndogo, ni ganda la risasi arobaini na nane, urefu kama *huo* tu, risasi .22 ya kawaida. Inaposhindiliwa ina nguvu karibu ya .30-06. Sasa ni . . . Kiwanda hushindilia tu hizo kwa karibu futi elfu nne na mia nne kwa sekunde. Vema, lakini waweza kuweka za kutosha . . . ulishindilie wewe mwenyewe, na unaweza kuweka hata futi elfu tano kwa sekunde. Na—na la sivyo, kama unafyatua risasi . . . Tulikuwa tukipiga bunduki, hivi majuzi, yadi mia mbili, na risasi ile ingalianguka chini, ingaliruka kabla bunduki haijarudisha mwangwi. Hivyo ndivyo inavyoruka upesi.

846 Ndipo uchukue kijiti cha kuchokoa meno (mwajua ile sehemu yake pana) na kukisukumiza barutini na kujaza kitu hicho baruti, karibu tu punje ndogo nne au tano, na kuiweka juu pale, ndiposa weka risasi ndani pale. Simama hapa, nawe uchukue risasi mkononi mwako katika muda wa sekunde moja. Na kumpiga risasi nguruwe mwitu nje pale walikoketi umbali wa futi mia mbili kutoka kwako, na yule nguruwe hata hakujimudu. Risasi zile hugeuka na kuwa katika hali yake ya asili, katika gensi. Hapa kuna risasi ambayo ni mchanganyiko wa shaba nyekundu na bildi, na kwa nukta moja, imerudi tena hata hutaipata tena. Ilirudia asili yake miaka bilioni mia iliyopita, kurudia gensi. Gensi hizo hazina budi kutengenezeka ziwe tena shaba nyekundu na bildi, na vinginevyo kama hivyo. Gensi hizo hazina budi kudidimia.

847 Naam, basi. Hivyo ndivyo tulivyo hapa, tunatoka kwa viumbe bora zaidi. Hapo mwanzo tulikuwa katika mfano wa Mungu. Utaji na giza vinatuzuia tusijue hilo sasa. Lakini Yesu aliwaambia wanafunzi Wake ya kuwa Yeye "alikuwa nao kabla kuwekwa misingi ya dunia." Ona? Tulikuwako! Huwezi kulijua hilo sasa, lakini ulikuwako hapo mwanzo. "Na nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikaharibiwa, tunalo jengo linalotungojea!" Haleluya! Na tutakapoingia katika huu mwili wa Kiungu, tulimokuwa wakati mmoja, ndipo tutakula na kuamkuana kwa mikono. Na zile roho chini ya madhabahu hulia, "Hata lini, Bwana."

848 Kunazo hatua saba ziendazo kwa Mungu, kwa ajili ya wale Roho saba wana—wanaposhuka chini. Vema, uendapo chini ya madhabahu ya Mungu, hao wanalia, "Hata lini, Bwana?" Je, twaweza kurudi? Wako chini hapa.

849 Mungu alisema, “Basi muda mchache tu, hata wajoli wenu watakapoteswa kwa jambo lile lile ambalo mmeteseka kwalo.” Ona?

850 Ndiposa zile roho zitarudi, nazo zitakuwa wanaume na wanawake tena, na kuishi milele wakati giza lote na mauti na magojwa na huzuni ya weusi vimetoweka: hamna kivuli tena, ni nuru ya jua pekee!

851 Sikiza. Jambo ni hili. Hebu na kuwe giza kuwezavyo kuwa; hakuwezi kuwa giza sana hata jua litatowesha kila chembe ya giza hilo. Giza na nuru haviwezi kukaa pamoja. Kwa kuwa. . .Ipi ina nguvu zaidi? Ni nuru. Na nuru iangazapo, giza hutoroka. Amina. Je, hamna furaha? Je, hamna furaha sasa ya kwamba mnajua? Bila shaka, hamna kivuli ko kote. Lakini hii Nuru iliyobarikiwa iliyo moyoni mwetu hivi sasa, kitu fulani kinashuhudia: Mwana wa Mungu, ile nguvu ya Mungu.

852 Nasi tunakuja hapa, tunatazama uweza wa Roho Mtakatifu ukishuka na kuwaendea kusanyiko, na kusema, “Wewe ulikuwa Bi. *fulani*, kwamba ulifanya jambo *fulani*, mahali *fulani*. Umepata mapigo haya kwa muda mrefu, lakini BWANA ASEMA HIVI, ‘simama kwa miguu yako, umeponywa.’” Na kiwete na kipofu wanasimama kwa miguu yao. Na hicho kivuli cha mtu, aliyeliwa na kansa, kinapata nafuu na afya mpya tena.

853 Si ajabu, Yesu alisema, “Mambo haya nifanyayo Mimi, nanyi mtayafanya.” Naye akasema, “Sitendi lo lote asiponionyesha Baba yangu.”

854 Hiyo ni nini? Hiyo ni Nuru inayokuja imechanganyika na giza hili, mwaona, kutukomboa. Mwafahamu ninalokusudia?

855 Sasa, hivi karibuni itarudi nyuma kule, ndiposa huo mwili wa Kiungu utakuwa tena mwili usiokufa kama ilivyokuwa hapo mwanzoni, basi Yesu atakuja, na Mungu. . .Kristo watakapokuwa mmoja, Kristo ataketi kwenye kile Kiti cha Enzi na watu wote watakuwa wanadamu. Kristo atakuwa kwenye kile kiti cha enzi cha Daudi, mwanadamu, Bwana Yesu: hamna mauti tena. Hatutakufa tena kamwe, hatutaugua tena, hutahuzunika tena, nasi tutaishi katika kile kipidi cha miaka elfu.

856 Na ile miaka elfu itakapokwisha hapa duniani, ndipo Shetani atakuja; na ule ufufuo wa pili utakuja; ule ufufuo wa walio waovu. Watakusanya jeshi kubwa kama mchanga wa bahari, nao watakuja kuzingira marago ya watakatifu; na hayo yatakapotendeka, Mungu atanyesha moto na viberiti toka mbinguni na kuwaangamiza.

857 Naye Yohana alisema, “Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya: kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena. Nami, Yohana, nikauona ule Mji Mtakatifu, Yesusalaemu Mpya, ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi—arusi aliyekwisha—kupambwa kwa mumewe.” Naam.

858 Pale yeye alisema, "Bibi...Mwana-Kondoo na Bibi-arusi watakuwa pale milele." Kutakuwako dunia mpya, mamilioni na mamilioni ya maili mraba. Jamani. Mji ule, Biblia iliupima Mji ule wa maili elfu kumi na tano mraba. Ni urefu wa maili elfu kumi na tano upana wa maili elfu kumi na tano, na maili elfu kumi na tano kwenda juu. Hayo ndiyo maelezo hasa ambayo Biblia inatoa juu ya Mji huo. Si ajabu hapana bahari tena, Hapakuwepo nafsi kwake.

859 Ee, kutakuwa kuzuri jinsi gani! Na ndani mle, kuna chemchemi papo hapo penye kile Kiti cha Enzi cha Mungu, kitiririkacho mbele ya kile Kiti cha Enzi. Kuna mti pande zote mbili za ule mti...za ule mto wa Uzima. Na katika mti huu mnakaa maombi...aina kumi na mbili ya matunda, na wenye kutoa matunda yake kila mwezi.

860 Mna wale wazee ishirini na wanne. Mna Bibi-arusi. Mna wale mia na arobaini na nne elfu, wale matowashi wa hekaluni. Ewe Ndugu, tunakwenda mahali penyewe! Mambo ya ajabu yamo mbele kwa ajili yetu. Wale wanne... Wale wazee ishirini na wanne. Wale matowashi mia na orobaini na nne elfu. Bibi-arusi akiketi pamoja na Kristo. Lo, mwanena...Nyumbani kwangu, Nyumbani kuzuri! Amina.

861 Kuwaza kuwa nina majaliwa ya kwenda kule, nawe una majaliwa ya kwenda kule. Na mbona uchague kutembea katika giza hili na usione Nuru, na ufe na kwenda katika ghasia na kuangamia? Kwa kuwa Nuru inapotawala, giza halina nafasi. Katafute giza lilipokwenda nuru ilipokuja. Hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati vitu vyote vitakaporudishiwa Mungu humo. Giza lilikuwa na mwanzo, giza lina mwisho. Nuru haikupata kuwa na mwanzo wala haitakuwa na mwisho kamwe. Mungu hakuwa na mwanzo wala hana mwisho. Kwa hivyo, siku moja, ulimwengu wote mpotovu pamoja na dhambi zake zote na urembo wake, unavyoitwa, na mazuri yake yote na miamsho, na uzuri wake wote wa kudanganya na kadhalika vitafifia hata vitokomee, na havitakuwako tena. Havitakuwako tena, havitawaziwa tena! Ilisema, hata, "Hata havitakumbukwa tena."

862 Lakini wabarikiwa wa Bwana watakuwa pamoja Naye daima. Tutakuwa na mwili kama Wake uliotukuzwa, na kuishi pamoja Naye na kula pamoja Naye na kukaa pamoja Naye, na kuishi pamoja Naye milele na kwa wakati usio na kikomo; na nyakati za Milele zitaendelea pamoja na ulimwengu usio na mwisho.

863 Nawe una chaguo usiku huu. Kama hujajitayarisha kukabilia mahali hapo, haijalishi unaenda kanisani mara ngapi, u mshiriki mzuri vipi, umepotea hata Kristo atakapokupa wewe Uzima mpya katika giza hilo unalotembelea. Huenda ukawa wa kidini. Wa kidini...Vema, sikiza rafiki, dini ni elimu. Ona?

Watoto wote wa Kaini daima walikuwa na dini. Wayahudi walikuwa na dini Yesu alipokuja, bali waliukataa wokovu.

864 Huenda ukawa wa kidini sana usiku huu. Huenda u Mpresbiteria, Mmethodisti, Mpentekoste, Mnazarini, Mpilgrim Holiness. Huenda ukawa tu wa dini, unaenda kanisani na kushuhudia, huenda ukaimba na kupiga shangwe na kumsifu Bwana, huenda ukaleta fungu lako la kumi kanisani, huenda ukamtendea jirani yako mema, hayo hayahusiani kamwe na kituo chako cha Milele. Kaini alifanya kila moja ya hayo. Hakika.

865 Biblia ilisema kuwa "ngano na magugu yalikuwa pamoja." Maskini ile ngano ikakaa, inaumia kwa njaa ya mvua, na ile—ile miimba pia. Mvua ilipokuja, miiba ikafurahi tu kwa kupata mvua kama ngano nayo. "Lakini, ni kwa matunda yao, mtawajua."

Sasa hebu tuombe huku mnapochunguza matunda yenu:

866 Sasa, Baba, Mungu, kumekuwa na maswali kadha magumu hapa usiku huu. Huenda sijafanya jambo linalofaa, bali kwa kadiri nijuavyo mimi; wajua moyo wangu. Naomba, Mungu, ya kuwa utaipokea. Na sasa labda katika baadhi ya maswali haya, kama sikuyajibu ipasavyo, basi na uongee na mioyo ya watu, na uiweke ipaswapo kuwa. Nahisi kwamba uliniambia mimi. Lakini kama ningekosea, basi unisamehe.

867 Nami naomba, Mungu, kuwa kila mmoja wa hawa ataweka mambo haya moyoni mwake, nao na wayatafakari na kuwaza hivi, "Naam kanisa ndilo hilo, mambo hayo ndivyo yalivyo. Hivyo ndivyo Biblia ilisema."

868 Labda hawa mabibi Bwana, Wewe unajua sikukusudia kitu cho chote kibinafsi kwa kuwaambia. Lakini, Mungu, na—nawapenda dada zangu, nawe wajua hilo, Baba. Wajua ninayowaza juu yao. Bali ningalisimama na kuwaambia kitu fulani kisicho sahihi, ningekuwa m—mdanganyifu kwao. Situmai kuwa mdanganyifu kwa dada zangu, nataka kuwaambia yaliyo Kweli. Na, Baba, nayatoa moja kwa moja toka kwa Neno Lako.

869 Naam, siwalaumu ndugu zangu, lakini Bwana, nasema kuwa wamekosea kwa kuruhusia mambo haya. Na kama mwanamke angejua vingine na kuendelea na kufanya hivyo, basi ni juu yake, mchungaji yule hana hatia.

870 Abba Baba, mambo hayo ni Neno Lako, na ni juu Yako. Sasa nena na mioyo ya watu hawa. Nawakabidhi wote Kwako. Nitaona yale umetenda, Baba; wajua. Neno kwa kila moyo. Twaomba katika Jina la Kristo.

Na hali vichwa vyetu vimeinamishwa:

871 Nashangaa kama mtu ye yote angeinua mkono wake, kaseme "Ndugu Branham, hebu nikumbuke mimi ili niweze kuwa

mshindi kabisa, na siku ya mwisho nipate kuvaa ile nguo ya arusi na niwe pamoja na Kristo." Je, waweza kuinua mkono wako, useme, "Niombee mimi"?

872 Kila mtu ainamishe kichwa chake sasa, na kiinamishe tu. Mungu akubariki, hilo ni zuri. Pale, Mungu awabariki, dada zangu na ndugu zangu, pia mnaoinua mikono yenu. Hilo ni ajabu.

873 Sasa, Baba, umeona mikono yao. (Najua, wakati mwingine unafikiri, "Vema, ombi ndogo tu hovyo?") Mungu, nawaza kuhusu mama yule, aliyesema jana, "Ombi ndogo tu pale katika nyumba yake siku hiyo wakati mvulana yule alikuwa yu afa, majuma matatu tu ya kuishi, ule ugonjwa wa kufisha kwenye ubongo, na sasa mabadiliko yakaja."

874 Nawaza kuhusu Hezekia, akiegemeza uso wake kuelelea ukuta ule na kulia, "Bwana nakusihi, unirehemu. Nikumbuke, kwa kuwa nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu." Iligeuka kutoka kwa kifo hata uhai.

875 Kupaza sauti tu kumoja kwa Mwana wa Mungu. "Lazaro, njoo huku nje!" na mtu aliyekufa akafufuka.

876 Ee Mungu, ulisema, "Nena, omba, na utapewa. Usemapo lo lote, amini ya kwamba lile usemalo litatimia, nawe utapata lile usemalo."

877 Sasa, Baba naomba kwamba kila aliyeinua mkono wake atapokea kile walichokiinulia mkono. Nao wabarikwe. Mungu, naomba ya kwamba utawasaidia dada zetu, ili wao wawe... nao waenende iwapasavyo, ili Shetani kupitia kwa televisheni na magazeti ya *Hadithi ya Kweli* na kadhalika ambayo yamechapishwa ovyo—ovyo, na vipindi visivyochunguzwa, jinsi mambo machafu ya kishenzi kwenye televisheni na kadhalika, ambayo inge... Vingekuwa vifaa vya kuleta mamilioni ya watu Kwako, lakini jinsi havichunguzwi hapo kabla, na kuondoa vitu hivi vichafu ambavyo hao... Ee, ni huzuni vipi? Na kujua kuwa roho wa Shetani ameingia na kuwazingira dada zetu, na wanajaribu kuwaonyesha mitindo na mavazi kama hayo.

878 Nasi twaona kuwa katika... katika ndugu zetu, pia Bwana, jinsi hao waoneleavyo waweza kuvuta sigara, kunywa pombe na kutenda yasiyofaa, na eti wangali Wakristo kwa kuwa hao husema "Wanaamini." Hebu nao wajue kuwa, "Shetani aamini pia." Naye hajaokoka bado, "Yeye anaamini na kutetemeka."

879 Na sasa, Baba, twaomba kuwa utaturehemu sisi sote, na kutusamehe dhambi zetu, labda wengine hawakuinua mikono yao, Ee, Mungu uwarehemu. Na wakati mwingine wapatapo nafasi na wainue mikono yao.

880 Tunajitayarisha kupokea ushirika, Bwana. Utusamehe makosa yetu pamoja na maisha yaliyopita. Nasi tupokee baraka Zako kwa kuwa twaomba katika Jina la Kristo. Amina.

881 Bwana awabariki. Nasikitika kuwakawisha hivi. Nashangaa, kabla tu ya ushirika, kama kunaye ye yote aliyekuja kuombewa, angehitaji kuombewa, vema, tungefurahi kufanya hilo wakati huu, kama kuna ye yote atakayeombewa.

882 Vema, ndugu mlete mwanamke huyo hapa, naam. Tulieni kwa dakika chache, ndiposa tuta—tutawaruhusu mwende. Kisha tunapomruhusu kwenda, ndipo wale watakaotaka kubaki kwa ajili ya ushirika wanaweza kubaki. Lakini hivi sasa tutaombea wagonjwa. Biblia ilisemaje?

883 Kama ndugu huyo hawezi kuamka . . . Ni sawa, hebu aketi tu pale, tutamjia. Sawa, hebu tu aketi papo hapo. Nasi tutakuja chini pale na kumwombea. Sawa. Vema, bwana, hebu tu—hebu yeye aketi papo hapo. Ni vigumu kwake kusimama hapa, naam, tutafurahi kuja kwake.

884 Sasa nataka kutaja hili jambo ndogo, rafiki yangu mpendwa. Ona, ni—ninajua kuwa Bwana amethibitisha hili mara kwa mara, mara nyingi sana. Ona? Mimi si mhubiri bora, sina elimu na kadhalika. Nampenda Bwana Yesu, Mungu ajua nampenda. Lakini jambo moja nilililoitiwa ni kuombea wagonjwa. Je, waamini hilo? Hata kabla sijajua kuhusu kipawa kile, nilikuwa nikienda hapa hospitalini, nami nakumbuka hao wauguzi wakisema, "Sasa utapona." Ona? Na ni ajabu, kwamba Mungu kwa hisani Yake amejibu maombi yangu kwa watu.

885 Nawaza, usiku huu, kama wangaliitwa, mbiu ya dunia nzima kila mahali duniani. Na isemwe, kila mtu ambaye Ndugu Branham amemwombea, njoo hapa, ningependa muipashe habari serikali ya Marekani, kwa barua. Na hilo liwe tangazo la redioni kote ulimwenguni. Nakisia, Ona? Nakisia, labda watu milioni nne milioni tano wangejibu mbiu hiyo kama ilijulikana.

886 Na watu hao, au baadhi yao walikuwa wamekwisha kufa, wamekatiwa tamaa na daktari, na—na mzishi. Wengine wao wameuawa katika ajali; wengine wao walikufa kifo cha kawaida. Wengine wao ni vipofu waliopooza, viwete, waliopindika, walioteseka, wenda wazimu . . . mahospitalini, hata hawakujua tulikuwa hospitalini kuwaombea. Tukawaingiza ndani, ilitulazimu kuwachukua. Wangepigana kote kote na kujikatakata vipande vipande, bila hata kujua yeye alipo. Katika dakika tano, hajambo, mtu mzuri, mpenda watu, na mwenye akili timamu siku zake zote zilizobakia. Ona?

887 Ni . . . Ni nini? Si Ndugu Branham. Ni Yesu Kristo, Yeye alinituma mimi kuwaombea wagonjwa. Naam, jambo ni hili, Hakijapata mafanikio makuu Jeffersonville, kwa kuwa, hii ndiyo sababu. Sasa, nawatakeni mjue nina baadhi ya marafiki wasiri wangu na marafiki wazuri walio hapa katika mji huu. Ingawa mji wenyewe, hali ya mji huu, siipendi. Siipendi hali hii, na sijawahi kuipenda; nilipokuwa mvulana mdogo, nimeketi,

nikisoma vitabu vyangu vya historia, nilisema, wakati mmoja nitaondoka hapa." Ona?

888 Siipendi Jeffersonville, ni maji-maji, iko chini humu. Ni maji maji sana na—na ni mbaya sana. Nenda juu hapa juu ya Spickert Knobs au po pote pale, na utazame chini kuelekea New Albany na Jeffersonville, ukitaka kuona. Tazama, hata madaktari wanasema sasa, kuwa, "Watu wa bonde hili wanapata ugonjwa wa kukosa damu kwa sababu ya hali hiyo."

889 Maskini mwanamke mmoja hapa, Bi Morgan, aliponywa kansa, akampeleka mbwa wake hapa kwenye zahanati, alidhani huyo mbwa alikuwa na upele. Mwajua ilikuwa nini? Kudidimia kwa Colgate na kadhalika kwenye magugu aliyokanyaga. Ni mahali pasipo na afya kabisa.

890 Mtu fulani alikuwa Jeshini, akashuka akaenda hapa na kupata. . .Akaambukizwa na pumu. Alienda kule Florida na macho yake yakawa meusi sana, naye akamwendea daktari, akasema, "Daktari . . . "

891 Daktari akasema, "Sasa, umekuwa ukipigana, sivyo?"

892 Akasema, "La, bwana, sivyo."

893 Mkitaka kujua ni nani jina lake ni Herby. Sasa, kama nikiweza kuwazia tu. . .Ni—ni katika Shirika la Benki ya Taifa katika New Albany, yeye ni mwenye kuhesabu fedha. Nenda kule kamwone mtu aitwaye "Herby," ukamuulize.

894 Na yeye alisema. . .Alikwenda, yeye alisema, "Daktari," yeye akasema, "Nina homa ya mapindi."

895 Naye alimchunguza, kasema, "Naam." Akasema, "Nilidhani umetoka kupigana." Kasema, "Kijana, unaishi wapi."

896 Akasema, "Huenda sasa ukajua mahali pale," kasema, "Naishi katika mji mdogo unapopita Louisville, Kentucky, unaoitwa New Albany, Indiana."

897 Kasema, "Unakusudia kuniambia mimi kuwa umepata homa ya mapindi kutoka kwa maji haya ya chumvi hapa Miami, ukija?" Akasema, "Kama unaweza kuishi katika Jeffersonville, Indiana, au New Albany, Indiana, ungeishi ko kote ulimwenguni ambako jeshi la Amerika lingekupeleka." Hivyo tu. Ona?

898 Ni mahali pasipo na afya sana ulimwenguni, nipajuapo, ijapokuwa iwe katika bwawa la malaria. Ona? Na ni—ni—ni—nina marafiki hapa.

899 Tazama hapa, naweza tu kwenda kuwaita hivi. Mtazame Dk. Sam Adair, msiri wangu. Vema, kuna Mike Egan, anayeketi hapa. Jamani, ningewataja wangapi! Mamia tu ya marafiki wasiri wangu, rafiki zangu wa kale, wenzangu. . .Haijalishi ni marafiki wapya wangapi nipatao, hakuna cho chote kitakachopachukua mahali pa marafiki wangu wa kale.

900 Ndiye huyo mama yangu mzee anayeketi nyuma kule, hana siku nyingi duniani, yeye ako katika miaka yake ya sitini na kitu sasa. Ndiye huyo mama mkwe wangu, miaka sabini, anaelekea sabini na mmoja; ameketi nyuma hapa mahali fulani nadhani, usiku huu. Na pale nimwache. Baba yangu alizikwa juu hapa; mke wangu alizikwa nje hapa Walnut Ridge; mtoto wangu amelala pale. Mwaona ninalokusudia?

901 Si—si—sipendi . . . si—sisitaki kukaa hapa, nami naamini kuwa hivi punde, hivi karibuni sina budi kuondoka. Ona, kwa sababu imekuwa ikinijia, nasema hili mimbarani pamoja na Biblia yangu, mara kwa mara.

902 Nilipomwambia mke wangu, walipotupa pesa za kujenga jumba hilo la mchungaji ambalo nililirudishia kanisa hili . . . Kanisa hili linamiliki hiyo nyumba yaa mchungaji; nenda chini hapa, chunguza kama sivyo. Ona, singelilitwaa mwenyewe.

903 Sasa, nilipokuwa naenda kujenga pale, Meda alisema, "Nataka kuishi hapa kwa ajili ya mama yangu."

904 Nilisema, "Mpenzi, bila shaka tukifanya hivyo, tutajuta kwake. Ona, haiwezekani. Mungu amesema, 'Jitengeni', yanipasa kufanya hivyo."

905 Na kasema, "Vema, mama yangu!"

906 Nilisema, "Mama yangu pia. 'Lakini yeye asiyetengana na walio wake, na kunifuata Mimi, hastahili kuitwa Wangu.' Na hilo ni kweli."

907 Hivi karibuni, hivi punde, naona itanibidi kuondoka, yaani, kuhama. Lakini hii ndiyo sababu, mikutano haifanikiwi hapa. Haitafanikiwa jinsi ilivyo kwingineko, na ye yote aliyewahi kuwa mikutanoni ajua hilo ni kweli kwa sababu ni papa hapa katika mji wangu mwenyewe. Naam.

908 Yesu alisema jambo lile lile alipokuja,

909 Walisema, "Mtu huyu ni nani? Je, huyo siye yule kijana wa seremala hapa? Alisomea shule gani? Alipata wapi elimu yake? Sasa hebu nikuone ukitenda . . . Ulisema ulitenda miujiza humu, hebu nikuone ukitenda jambo lile hapa. Yale uliyotenda kule Kapernaumu, hebu nione ukiyatenda hapa."

910 Yesu alisema . . . "Yeye alishangazwa na kutokuamini kwao." Aligeuka na kusema, "Amin, Amin nawaambieni, hakuna nabii mwenye kukubaliwa miongoni mwa watu wake na katika nchi yake mwenyewe." Sivyo?

911 Nasi twajua . . . tazama . . . Chukua Finney, chukua Sankey, Moody; chukua John Wesley, hangefanikiwa kamwe, ona, hata alipoondoka katika nchi yake. Mtazame—mtazame—mta—mtazame Moody. Wakati Moody, mtengeneza viatu wa Boston, hangeendelea kwa vyo vyote vile, yeye alikuja Chicago kabla hajawa mashuhuri. Ona? Ilimpasa kuwaondokea walio wake. Inakupasa kufanya hivyo kila mara.

912 Lakini sasa, hapa, Mungu atajibu maombi kama utasahau ni William Branham; ona, kama utasahaukuwa William Branham anahusika nayo, ni mtu tu anayesimama na kuwaombea tu. Yesu Kristo ndiye ambaye amekwisha kufanya yale uliyoomba akufanyie, kama utaliamini tu. Ona? Haihusuani. . .Sihusiki kamwe, ni kushuhudia tu. Lakini inaonekana kama baada ya kukulia hapa pamoja nanyi, nanyi mwajua kila udhaifu nilio nao, na kila kosa nililo nalo. . .Nanyi mwajua yale Mungu amefanya, papa hapa mjini.

913 Mji huu, katika Siku ya Hukumu, utapata hukumu kali hivi karibuni, kwa kuwa kumekuwa mamia na mamia ya uponyaji wa ajabu sana hapa. Naam, papa hapa. Ishara na maajabu, na kuonekana kwa yule Malaika chini pale, na magazeti yalitangaza na kadhalika, ingawaje, watu hawa. . . Mbona hivyo?

914 Sasa, hivi karibuni nitaondoka hapa. Nashangaa "Mwisho wangu utakuwaje?" Imekwisha? Imekaribia sana kwisha? Nina umri wa miaka arobaini na minane. Karibu kwisha? Nashangaa, kama ndivyo.

915 Tazama, mbona ulimwengu haukuitambua ile picha pale? Mbona hao hawakuielewa upesi sana? Mbona hawafahamu mambo hayo mengine? Mbona hawazifahamu nabii hizi na kadhalika? Mnajua, hawawezi sasa, bali siku moja nitaondoka duniani na niondokapo, basi wataitambua. Baadhi yenu vijana mtaitambua nikiisha kuondoka. Ona? Bali Mungu hangeruhusu ifanyike sasa.

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org